# MUHTASARI WA **RIPOTI YA HAKI ZA BINADAMU TANZANIA 2022**

## Safari ya Maboresho ya Mfumo wa Haki Jinai Kulinda Haki za Binadamu



HAKIUZWI

LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

75 UNIVERSAL DECLARATION OF HUMAN RIGHTS
DIGNITY, FREEDOM & JUSTICE FOR ALL

Zanzibar Fighting Against Youth Challenges Organization
ZAFAYCO

**Mwandishi:**
Bw. Fundikila Wazambi

**Wahariri:**
Dkt. Anna Henga
Bi. Felista Mauya

**Mchapishaji:**
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
Machi 2023

**HAKIUZWI**

**ISBN: 978-9987-740-69-1**

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| **Kuhusu Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu** | **ii** |
| **Muhtasari** | **iii** |
| **SURA YA KWANZA:** KUHUSU TANZANIA | **01** |
| **SURA YA PILI:** HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA | **06** |
| **SURA YA TATU:** HAKI ZA KIUCHUMI, KIJAMII, NA KIUTAMADUNI | **28** |
| **SURA YA NNE:** HAKI ZA KIUJUMLA | **40** |
| **SURA YA TANO:** HAKI ZA MAKUNDI MAALUM | **44** |
| **SURA YA SITA:** MIFUMO YA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU | **68** |
| **SURA YA SABA:** UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA RIPOTI ZILIZOPITA ZA HAKI ZA BINADAMU | **72** |
| **SURA YA NANE:** HITIMISHO NA MAPENDEKEZO | **76** |

# KUHUSU KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

LKituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni shirika binafsi, huru, la hiari, lisilo la kiserikali, lisilofungamana na chama chochote cha kisiasa na lisilotengeneza faida kwa ajili ya kugawana, ambalo linalenga kufikia jamii yenye haki na usawa. LHRC ina lengo la kuwawezesha Watanzania kukuza, kuimarisha na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini. Lengo kubwa la LHRC ni kujenga ufahamu wa sheria na haki za binadamu miongoni mwa umma na hasa watu walio katika hatari kubwa ya haki zao za msingi kukiukwa, kutoa elimu ya sheria na uraia, kufanya utetezi unaohusisha pia msaada wa kisheria, pamoja na kufanya utafiti na ufuatiliaji wa haki za binadamu. LHRC ilianzishwa mwaka 1995 na inafanya kazi Tanzania Bara.

# MUHTASARI

- Utoaji wito zaidi wa maboresho ya mfumo wa haki jinai
- Kupitishwa kwa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa 2021-2024.
- Kuanzishwa kwa kikosi kazi cha kuwalinda watoto dhidi ya usafirishaji haramu wa binadamu.
- Kufanyika kwa sensa ya taifa ya watu na makazi katika maeneo yote nchini Tanzania.
- Sakata la tozo za miamala ya simu na namna lilivyoleta mijadala kuhusu haki za binadamu na kodi.
- Mgao wa maji na ukatikaji wa umeme na athari zake kwa haki za kiuchumi na kijamii.
- Kutolewa kwa Mwongozo wa Makubaliano ya Kukiri Kosa
- Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutangaza kufanya uchunguzi wa utaratibu wa makubaliano ya kukiri kosa.
- Serikali kutangaza nia ya kufanya mapitio ya sera ya elimu.
- Kuundwa kwa kikosi kazi cha kirais cha kuratibu maoni kuhusu demokrasia ya vyama vingi nchini Tanzania.
- Hukumu ya Mahakama Kuu kuhusu haki ya wafungwa na mahabusu ya kupiga kura, ambayo ipo kwa mujibu wa Katiba.
- Maamuzi ya Kamati ya Wataalamu wa Kiafrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto kuhusu upimaji wa lazima wa mimba na ufukuzaji shule wa wasichana wanaokutwa na mimba shuleni au walioolewa.
- Serikali kutangaza kuanza kwa mchakato wa kurekebisha Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016.
- Kuanzishwa kwa kamati ya watu 12 ya kuchunguza utendaji wa taasisi za haki jinai nchini, ikiwemo kuishauri Serikali namna bora ya kuboresha mfumo wa haki jinai.
- Kutungwa kwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2022.
- Wito wa wadau mbalimbali wa kuondolewa katazo la mikutano ya hadhara ya kisiasa.
- Kufunguliwa kwa vyombo kadhaa vya habari ambavyo vilifungiwa miaka ya nyuma.
- Kuletwa kwa Waraka mpya wa Viwango vya Chini vya Mshahara wa mwaka 2022.
- Mapendekezo ya kikosi kazi cha kirais cha kuratibu maoni kuhusu demokrasia ya vyama vingi nchini Tanzania ya matokeo ya uchaguzi wa urais kuweza kupingwa mahakamani, mara baada ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Juu.

# Dondoo Muhimu kwa Mwaka 2022

| | | |
|---|---|---|
| **1** | **Mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza** | • Mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza kuendelea kuwa tishio kwa haki za binadamu, ikiwemo haki ya kuishi, haki ya afya, haki ya kuwa salama, na uhuru dhidi ya ukatili.<br>• Matukio mengi ya mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza yanasababishwa na wivu wa kimapenzi.<br>• Wahanga wengi (zaidi ya asilimia 90) ni wanawake. |
| **2** | **Uhuru wa vyombo vya habari** | • Matumaini na mtazamo wa kuimarika kwa uhuru wa vyombo vya habari na matukio machache zaidi ya ukiukwaji wa uhuru huo kuripotiwa.<br>• Hata hivyo, bado sheria na kanuni zinazominya uhuru wa vyombo vya habari hazijarekebishwa.<br>• Pamoja na hali ya uhuru wa vyombo vya habari kuonekana kuimarika, Tanzania ilipanda kwa nafasi moja tu katika Viwango vya Uhuru wa Vyombo vya Habari vya mwaka 2022, huku alama zikishuka kidogo. |
| **3** | **Ukatili wa kichumi dhidi ya wanawake** | • Wasiwasi kuhusu upatikanaji, matumizi, na umiliki wa ardhi kwa wanawake wanaoishi vijijini.<br>• Changamoto ya wanawake na wazee kunyang'anywa mali na wanawake kuzuiwa kutumia kipato cha familia, hasa maeneo ya vijijini.<br>• Wajane kutolewa kinguvu nyumbani imekuwa jambo la kawaida, hasa maeneo ya vijijini na baadhi ya miji. Kufukuzwa na kunyang'anywa mali kunawaathiri sana wajane na watoto wao.<br>• Wanawake na wasichana kunyimwa haki ya kurithi na kumiliki mali bado ni changamoto.<br>• Mabadiliko ya kisheria yanahitajika kulinda haki za wanawake na wasichana za kurithi na kumiliki mali. |

| | | |
|---|---|---|
| **4** | **Haki jinai** | • Wito wa maboresho ya mfumo wa haki jinai nchini kuendelea kutolewa na wadau mbalimbali, ikiwemo Mh. Rais Samia Suluhu Hassan.<br>• Uundwaji wa kamati ya maboresho ya haki jinai hatua chanya kwa upande wa Serikali.<br>• Hata hivyo, jitahada za haraka zinahitajika kuboresha mfumo wa haki jinai nchini, kwani watuhumiwa wanaendelea kuteseka magerezani sababu ya changamoto mbalimbali, ikiwemo ucheleweshaji katika uchunguzi, uwekaji watuhumiwa kizuizini kwa muda mrefu, uahirishaji wa kesi mara kwa mara, na ucheleweshaji katika ukamilishaji wa kesi.<br>• Changamoto ya mazingira yasiyoridhisha gerezani.<br>• Wanawake waliofungwa na kuwekwa kizuizini kuathirika zaidi na mazingira yasiyoridhisha gerezani. |
| **5** | **Ukatili dhidi ya wazee** | • Wazee kushambuliwa na kuuwawa, ikiwemo na watoto wao wenyewe, kwa sababu mbalimbali ikiwemo imani za kishirikina na mali.<br>• Wazee, wanawake kwa wanaume, kufanyiwa vitendo mbalimbil vya ukatili, ikiwemo wa kimwili, kingono, kisaikolojia, na kiuchumi.<br>• Matukio ya ukatili dhidi ya wazee kuongezeka mwaka 2022 na kuwafanya waishi kwa hofu, hasa maeneo ya vijijini. |
| **6** | **Afya ya akili** | • Wataalamu wa afya kutaja afya ya akili kama changamoto kubwa mwaka 2022.<br>• Wagonjwa wa afya ya akili wamekuwa wakiongozeka katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.<br>• Afya ya akili chanzo kikuu cha kuongezeka kwa matukio ya watu kujiua katika sehemu mbalimbali nchini.<br>• Wahanga wengi wa kujiua ni wanaume na vijana. |

| | | |
|---|---|---|
| **7** | **Ukatili dhidi ya watoto** | • Ukatili tishio kubwa zaidi kwa haki za watoto.<br>• Ukatili wa kingono, hasa vitendo vya ubakaji na ulawiti, ndiyo aina ya ukatili wanaofanyiwa zaidi watoto.<br>• Ukatili wa kimwili dhidi ya watoto pia ni tatizo linalokua, ukifanywa zaidi na wazazi na walezi – ambapo wengi wao wamekuwa wakipendelea kutoa adhabu ya kuwaunguza watoto wao katika sehemu mbalimbali za miili yao.<br>• Mtazamo wa wanajamii wengi ni kwamba ukatili dhidi ya watoto ni tatizo kubwa katika jamii.<br>• Ukatili na unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto unaotokea katika taasisi za kidini, ikiwemo nyumba za ibada, kuonekana kuanza kuwa tatizo katika jamii. |
| **8** | **Ushiriki wa kisiasa** | • Jitihada za kuboresha demokrasia ya vyama vingi nchini ni hatua chanya katika kuimarisha ushiriki wa kisiasa.<br>• Haja ya kufanya maboresho kulinda haki ya ushiriki wa kisiasa wakati nchi ikijiandaa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.<br>• Marekebisho ya sheria za uchaguzi kuhakikisha ushiriki sawa wa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu katika siasa na uwakilishi katika ufanyaji maamuzi.<br>• Haja ya kufanya marekebisho ya kisheria kuondoa vikwazo vya kisheria vya ushiriki wa wanawake katika siasa, ikiwemo mianya ya kijinsia katika sheria za uchaguzi.<br>• Haki ya wafungwa na mahabusu kupiga kura kutetewa na Mhimili wa Mahakama.<br>• Mafunzo kadhaa kupatikana kutokana na uchaguzi wa hivi karibuni wa Kenya, ikiwemo matokeo ya urais kuweza kupigwa mahakamani, uhuru wa Mhimili wa Mahakama, uwazi, uhuru na uadilifu wa vyombo vya usimamizi wa uchaguzi, wadau kuruhusiwa kuhesabu kura, na haja ya Katiba mpya. |
| **9** | **Ubora wa huduma za elimu na afya** | • Wadau kuendelea kuonyesha wasiwasi kuhusu ubora wa elimu na kutoa wito wa mapitio ya mfumo wa elimu nchini.<br>• Changamoto ya ufinyu wa bajeti kikwazo kikubwa katika utoaji wa huduma bora za elimu na afya.<br>• Upungufu wa rasilimali watu katika sekta hizi muhimu pia bado ni changamoto kubwa na kikwazo katika utekelezaji na ufurahiaji wa haki za elimu na afya. |

| | | |
|---|---|---|
| **10** | **Uwezeshaji kiuchumi wa wanawake, vijina, na watu wenye ulemavu** | • Uwezeshaji kiuchumi ni muhimu katika kupambana dhidi ya ukatili wa kijinsia na kulinda haki za kiuchumi na kijamii, ikiwemo haki ya kufanya kazi na haki ya kuishi katika hali inayofaa.<br>• Programu ya uwezeshaji wa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu kiuchumi, kupitia mfumo wa halmashauri wa asilimia 10, imeleta matokeo chanya kwa makundi hayo, ikiwemo kutengeneza ajira na kujikwamua kiuchumi.<br>• Hata hivyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amegundua changamoto kadhaa katika utekelezaji wa programu hiyo, ikiwemo mikopo kutorejeshwa kwa ukamilifu, baadhi ya halmashauri kushindwa kutenga fedha kwa ajili ya programu hiyo kama inavyotakiwa kisheria, utoaji wa mikopo kwa vikundi visivyo na sifa, kutoafuata utaratibu wa kisheria uliowekwa katika utoaji wa mikopo, na uwezo duni wa baadhi ya maafisa maendeleo ya jamii katika kushughulikia mikopo. Uingiliaji wa kisiasa katika utoaji wa mikopo pia ni changamoto. |
| **11** | **Rushwa, Ubadhiribu, Uwajibikaji, na Maendeleo** | • Ripoti za hivi karibuni za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimeonyesha ukiukwaji mkubwa katika matumizi ya fedha za umma, ambao unaashiria vitendo vya rushwa na makosa yanayohusishwa na rushwa.<br>• Viashiria vya rushwa, ubadhirifu, na udanganyifu vilivyoonekana katika ripoti za hivi karibuni ni pamoja na matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kulipia bidhaa na huduma juu ya bei elekezi; matumizi mabaya ya ofisi/nafasi; malipo kwa wafanyakazi hewa; malipo kwa wakandarasi hewa; upokeaji wa bidhaa na huduma zilizo chini ya viwango; kukosekana kwa stakabadhi kwa baadhi ya malipo; kufanya malipo bila mkataba; kufanya malipo bila kupokea bidhaa au huduma; na kutofuata taratibu za manunuzi ya uma. |

# Muhtasari wa Hali ya Haki za Binadamu kwa Mwaka 2022

Kulingana na tathmini ya hali ya haki za binadamu nchini iliyofanywa na LHRC kwa kutumia viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, hali ya haki za binadamu ilionekana kuimarika kiasi kwa mwaka 2022 ukilinganisha na mwaka 2021. Kama ilivyokuwa kwa mwaka 2021, masuala na matukio mengi ya haki za binadamu yaliyoibuliwa na kuripotiwa yalikuwa ni ya ukiukwaji wa haki za kiraia na kisiasa.

## Haki 5 zilizokiukwa zaidi mwaka 2022

**01** **Haki ya kuishi**
*[Mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi; Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina; Mauaji ya wazee; Mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza]*

**02** **Uhuru dhidi ya Ukatili**
*[Ukatili dhidi ya watoto, hasa wa kingono; Ukatili dhidi ya mwenza; Ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu na wazee; Ukatili wa kimwili na kiuchumi dhidi ya wanawake]*

**03** **Haki ya Usawa mbele ya Sheria**
*[Kuwekwa kuzuizini kwa muda mrefu; Vikwazo vya ufikiaji haki m.f. rushwa]*

**04** **Haki ya kuwa Huru na Salama**
*[Uwekwaji kuzuizini gerezani kwa muda mrefu kusubiria kesi; Kunyimwa dhamana; Ukatili dhidi ya wanawake na watoto; Ukamataji na uwekaji kuzuizini watu kinyume na sheria; Ubambikaji wa kesi]*

**05** **Haki ya Elimu**
*[Ufinyu wa bajeti; Upungufu wa vifaa na nyenzo za kufundishia; Ubora; Mazingira ya kazi yasiyoridhisha kwa upande wa walimu; Ukatili dhidi ya watoto, ikiwemo ndoa na mimba za utotoni]*

# Mikoa iliyotajwa zaidi katika ripoti

Mikoa iliyotajwa zaidi katika ripoti kwa masuala ya haki za binadamu (chanya na hasi) na matukio ya ukukwaji wa haki za binadamu ni pamoja na: 1. Singida (179); 2. Kigoma (163); 3. Geita (140); 4. Dar es Salaam (139); 5. Njombe (124); 6. Dodoma (120); 7. Katavi (118); 8. Mara (114); 9. Mbeya (113); 10. Mtwara (112); 11. Tanga (108); 12. Iringa (106); 13. Kilimanjaro (103); 14. Arusha (100); 15. Shiyanga (86); na 16. Mwanza (81). Hii ina maana kwamba taarifa nyingi za hali ya haki za binadamu zilipatikana zaidi katika mikoa hii. Kwa upande wa kanda, mikoa ya Kanda ya Ziwa imejatwa zaidi (482), ikifuatiwa na Kanda ya Kati (432), Kadha ya Nyanda za Juu Kusini (397), Kanda ya Kaskazini (338), Kanda ya Magharibi (332), na Kanda ya Mashariki (331).





*Mikoa iliyotajwa zaidi katika Ripoti ya Haki za Binadamu 2022*




*Asilimia ya mikoa iliyotajwa zaidi katika Ripoti ya Haki za Binadamu 2022 kwa kanda*

# Wahanga wa ukiukwaji wa haki za binadamu

Kutokana na data za programu ya LHRC ya ufuatiliaji wa haki za binadamu za mwaka 2022, watoto ndiyo walikuwa wahanga wengi zaidi wa ukiukwaji wa haki za binadamu (asilimia 47), wakifuatiwa na wanawake (asilimia 33), wazee (asilimia 10), na watu wenye ulemavu (asilimia 4). Asilimia 6 iliyobaki ilikuwa ni wahanga wengine, ikiwemo wanaume.




*Wahanga wa ukiukwaji wa haki za binadamu kulingana na matukio yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2022*
*Chanzo: Programu ya Ufuatiliaji wa Haki za Binadamu mwaka 2022*

# MADHUMUNI YA RIPOTI NA MBINU ZA UKUSANYAJI DATA NA TAARIFA

## Madhumuni

**Elimu ya haki za binadamu**

haki fulani inamaanisha na kujumuisha nini? Haki hiyo inalindwa na mfumo upi wa kisheria? Kwa nini haki hii ni muhimu? Haki hii ina mipaka ipi?

**Kukumbushia**

ni maeneo gani ya haki za binadamu yanahitaji kuimarishwa?

**Uchechemuzi wenye ushahidi**

nini kinahitaji kubadilika na kwa nini?

**Mambo na matukio yaliyosaidia ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu**

ni mambo au matukio gani yameimarisha ulinzi au utekelezaji wa haki za binadamu?

**Mambo na matukio yaliyoathiri ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu**

ni mambo au matukio gani yameathiri ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu?

**Uchambuzi wa sheria na miswada**

ni nini kimebadilika kufuatia utungwaji wa sheria au marekebisho ya sheria au kanuni? Mabadiliko hayo yameleta au yataleta athari gani kwenye haki za binadamu?

**Mapendekezo**

nini kifanyike kuimarisha na kulinda haki za binadamu?

**Utoaji taarifa**

kutoa taarifa kuhusu haki za binadamu na masuala ya kisheria ili kuchukua tahadhari na kutekeleza wajibu wako kwa mujibu wa sheria mbalimbali za nchi.

**Kuonyesha mienendo**

hali ilikuwaje miaka ya nyuma ukilinganisha na sasa?

**Kutoa mwanga katika kupanga afua**

ripoti inaweza kutumika kama sehemu ya kuanzia katika kupanga afua mbalimbali.

**Kuelemisha**

kutoa elimu kuhusu haki za binadamu; elimu kuhusu mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu ya kitaifa, kikanda na kimataifa; elimu kuhusu masuala ya kisheria; elimu kuhusu mambo mapya kuhusu sheria na haki za binadamu.

# Mbinu za Ukusanyaji Data na Taarifa

Data na taarifa zilizotumika kuandaa Ripoti hii zilipatikana kupitia vyanzo vya awali na upili. Data na taarifa za awali zilipatikana kupitia Utafiti wa Haki za Binadamu 2022, ambao ulifanyika katika mikoa 20 ya Tanzania Bara, na programu za kituo, hasa programu za msaada wa kisheria na ufuatiliaji wa haki za binadamu. Data na taarifa za upili zilipatikana kupitia mapitio ya vyanzo mbalimbali vya kuaminika vya habari, ikiwemo ripoti za wadau wa kiserikali na wasio wa kiserikali, hotuba, na matamko mbalimbali. Pia, utafiti wa LHRC wa taarifa zilizotolewa na vyombo vya habari kwa mwaka 2022 ulitoa data na taarifa muhimu zilizosaidia uandaaji wa ripoti hii ya haki za binadamu, sambamba na kuwezesha ufanyaji wa utafiti zaidi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na sheria na haki za binadamu yaliyojitokeza katika taarifa hizo

# KUHUSIANA NA RIPOTI

Ripoti ya Haki za Binadamu ya Mwaka 2022 ni ripoti ya 21 ya haki za binadamu kuandaliwa na LHRC tangu shirika lilipoanzisha utaratibu huo mwaka 2002. Ripoti ya mwaka huu imeangazia hali ya haki za binadamu kwa pande zote mbili za Tanzania Bara na Zanzibar, ambapo Sehemu ya Kwanza imejikita kwa Tanzania Bara na Sehemu ya Pili imejikita Zanzibar. Ripoti imefanya tathmini ya hali ya haki za binadamu nchini kulingana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, na inajumuisha vizazi vyote vitatu vya haki za binadamu, ambavyo ni: haki za kiraia na kisiasa; haki za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni; na haki za kiujumla.

| | |
|---|---|
| **SURA YA KWANZA:** Utangulizi | Inaelezea kwa kifupi kuhusu Tanzania, ikigusia historia, jiografia, idadi ya watu na mihimili ya serikali, na wajibu wa mihimili hii katika ulinzi wa haki za binadamu. |
| **SURA YA PILI:** Haki za Kiraia na Kisiasa | Inaelezea hali ya haki za msingi za kiraia na kisiasa, ikiwemo uhuru wa kujumuika na kukusanyika; uhuru wa kujieleza; haki ya usawa mbele ya sheria na kupata nafuu ya kisheria; na haki ya kuishi |
| **SURA YA TATU:** Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni | Inaelezea haki muhimu za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, ikiwemo haki ya kufanya kazi, haki ya elimu, haki ya afya, haki ya maji safi na salama, haki ya kumiliki mali, na haki ya kuishi katika hali inayofaa. |
| **SURA YA NNE:** Haki za Kiujumla | Inaangazia hali ya haki za kiujumla, hususan haki ya maendeleo, haki ya kufurahia na kufaidika na rasilimali asilia, na haki ya mazingira safi na salama. |
| **SURA YA TANO:** Haki za Makundi Maalum | Inaelezea hali ya haki za makundi maalum, ikiwemo wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, na wazee. |
| **SURA YA SITA:** Mifumo ya Ulinzi wa Haki za Binadamu | Inaangazia mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu katika ngazi za kitaifa, kikanda, na kimataifa na kujadili wajibu wake katika ulinzi wa haki za binadamu. |
| **SURA YA SABA:** Utekelezaji wa Mapendekezo katika Ripoti Zilizopita | Inafanya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti zilizopita za haki za binadamu. |
| **SURA YA NANE:** Hitimisho na Mapendekezo | Inatoa hitimisho kuhusu haki za binadamu na kutoa mapendekezo yatakayosaidia kukuza na kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu nchini Tanzania. |



# 01

## SURA YA KWANZA:
# KUHUSU TANZANIA

# SURA YA KWANZA:
# KUHUSU TANZANIA

## 1.1. Historia

Kabla ya kutawaliwa na wakoloni wa Kijerumani na Kiingereza katika Karne ya 19, Tanganyika (sasa Tanzania Bara) ilikaliwa na wazawa waliokuwa wakizungumza lugha ya Kibantu, ambao baadaye walipata ugeni toka Bara la Asia na toka Uarabuni. Kufikia Karne ya 15 Wareno nao wakaingia; na katika kipindi hicho cha Waarabu na Wareno ndipo biashara ya utumwa ilipamba moto. Ilipofika mwaka 1880 ulifanyika mkutano mkubwa katika Mji wa Berlin – Ujerumani, ambapo nchi za Ulaya zililigawa Bara la Afrika kwa ajili ya kulitawala. Ujerumani ilipewa sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki, ikiwemo Tanganyika. Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, Tanganyika iliwekwa chini ya ukoloni wa Uingereza, mpaka ilipofikia mwaka 1961, ambapo Tanganyika ilipata uhuru. Katika kipindi chote cha ukoloni, machifu mbalimbali walipigana na uongozi kandamizi wa kikoloni, ambao ulikandamiza haki zao kama binadamu, akiwemo Mtemi Mirambo wa Wanyamwezi, Mangi Meli wa Wachagga na Abushiri wa Pangani. Mapigano makubwa zaidi yalitokea Mwaka 1905 wakati wa ukoloni wa Mjerumani, yakifahamika zaidi kama Vita vya Majimaji, ambavyo viliongozwa na kiongozi wa kimila na kiroho aliyeitwa Kinjekitile Ngwale, ambaye aliaminika kuwa na uwezo wa kugeuza risasi kuwa maji.

Harakati za kupata uhuru ziliongozwa na chama cha TANU (Tanganyika African National Union), ambacho kilizaliwa mwaka 1954, kabla ya hapo kikifahamika kama TAA (Tanganyika African Association), kilichoanzishwa mwaka 1929. Kiongozi wa chama alikuwa Mwl. Julius Nyerere, ambaye aliiongoza TANU na Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961, akiwa Waziri Mkuu wa Kwanza chini ya Katiba ya Uhuru. Mwaka 1962, Tanganyika ikawa Jamhuri, Nyerere akiwa Rais wake wa kwanza chini ya Katiba ya Jamhuri, ambayo ilimfanya kuwa Kiongozi wa Taifa, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu, pia akiwa

sehemu ya Bunge. Mwaka 1964, Tanganyika iliungana na Zanzibar, ambayo ilikuwa imepata uhuru toka kwa Sultani wa Oman mwaka 1963, na kuunda Tanzania. Katiba ya tatu, Katiba ya Muungano, iliundwa, ikileta mfumo wa serikali mbili, chini ya vyama vya TANU (Tanzania Bara) na ASP (Zanzibar). Mwaka 1965, Katiba ya Mpito iliundwa, ambayo ilirudisha nchi katika mfumo wa chama kimoja. Katiba hii ilipitishwa kama sheria nyingine za bunge, kinyume na kanuni za kikatiba. Mwaka 1977, vyama vya siasa vya TANU na ASP viliungana na kuunda Chama cha Mapinduzi (CCM), ambacho kilitengeneza Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ambayo ndiyo inayotumika mpaka leo, japo imekuwa ikifanyiwa marekebisho mbalimbali yapatayo kumi na nne mpaka mwaka 2015. Mojawapo ya marekebisho makubwa ni yale ya mwaka 1992, ambayo yalirudisha mfumo wa vyama vingi. Mengine ni yale ya mwaka 1984, ambayo hatimaye yaliingiza hati ya haki za binadamu kwenye Katiba. Kabla ya hapo, tangu nchi ipate uhuru, haki za binadamu hazikuonekana kuwa muhimu sana kujumishwa kwenye Katiba, japo Tanzania ilikuwa imeshaanza kuridhia baadhi ya mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu.

## 1.2. Jiografia

Tanzania iko kati ya Latitudo 10 na 120 Kusini na Longitudo 290 na 410 Mashariki. Inapakana na Bahari ya Hindi upande wa Mashariki na imepakana na nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi na Zambia kwa pande nyingine. Tanzania ndiyo nchi kubwa kuliko zote Afrika Mashariki na ina Mlima Kilimanjaro, ambao ndiyo mlima mrefu kuliko yote barani Afrika na wa tatu duniani. Tanzania imebarikiwa kuwa na maliasili nyingi, ikiwemo mimea, mabonde ya ufa, maziwa, mito, na mbuga za wanyama. Maziwa ni pamoja na Ziwa Victoria - ambalo ni kubwa kuliko yote Afrika, na Ziwa Tanganyika - ambalo lina kina kirefu kuliko yote Afrika. Mbuga za wanyama ni pamoja na Serengeti, Mikumi, Manyara, Ngorongoro, na Katavi.

## 1.3. Idadi ya watu

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, idadi ya watu nchini Tanzania ni 61,741,120 (milioni 61.7), ambapo wanawake ni asilimia 51 na wanaume ni asilimia 49. Asilimia 96.9 ya watu ipo Tanzania Bara, na asilimia 3.1 iliyobaki ipo Zanzibar. Idadi kubwa ya watu ipo zaidi katika maeneo ya vijijini, ambapo pia idadi ya makazi ipo juu zaidi ukilinganisha na maeneo ya mijini.


## 1.4. Mihimili ya dola na wajibu wa mihili hiyo katika ulinzi wa haki za binadamu

Kuna mihimili mikuu mitatu ya dola nchini Tanzania, ambayo ni: Serikali, Bunge na Mahakama. Mihimili hii imeanzishwa na kupewa mamlaka na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

### A. Serikali Kuu

Serikali inajumuisha Rais - ambaye ni Kiongozi wa Taifa, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu - na Baraza la Mawaziri. Baraza la mawaziri linajumuisha Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar, na mawaziri wote. Rais ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri. Makamu wa Rais anamsaidia Rais kwenye mambo yote ya muungano. Zanzibar ina serikali yake na Rais wake chini ya mfumo wa serikali mbili ambao Tanzania inautumia, na ina mamlaka juu mambo yote ambayo siyo ya muungano, kama yalivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Wajibu katika ulinzi wa haki za binadamu:*** Wajibu wa Serikali Kuu ni pamoja na kutekeleza majukumu yake chini ya mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia; kuilinda Katiba, ambayo inajumuisha haki za binadamu; kuhakikisha utekelezaji wa haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kwa kutoa huduma za kijamii kama vile maji, afya na elimu; kulinda haki ya kuwa huru na salama kupitia vyombo vya dola na mifumo ya haki; na kutoa ulinzi wa kisheria na wa haki za binadamu kupitia Jeshi la Polisi, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na wizara husika katika sekta mbalimbali.



| Marais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| --- |
| Mw. Julius Kambarage Nyerere: 1964-1985 |
| Ali Hassan Mwinyi: 1985-1995 |
| Benjamin William Mkapa: 1995-2005 |
| Jakaya Mrisho Kikwete: 2005-2015 |
| John Pombe Magufuli: 2015- 2021 |
| Samia Suluhu Hassan – 2021 mpaka sasa |

**B. Bunge**

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo chombo kikuu cha kutunga sheria nchini, ambacho kinaundwa na wabunge mbalimbali wa chama tawala na vyama vya upinzani. Rais pia ni sehemu ya Bunge kwa mujibu wa Katiba. Kazi kuu ya bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Bunge hili lina mamlaka juu ya mambo yote ya muungano. Zanzibar ina Baraza la Wawakilishi, ambalo ndiyo chombo chake kikuu cha kutunga sheria na kuisimamia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Bunge lina wabunge wa kuchaguliwa na wabunge wa kuteuliwa.

***Role in human rights protection:*** Wajibu katika ulinzi wa haki za binadamu: Utungaji wa sheria za kulinda haki za binadamu; uridhiaji wa mikataba na utungaji wa sheria za kusaidia utekelezaji wa mikataba hiyo; kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa shughuli zake; kujadili masuala mbalimbali yanayohusiana na haki za binadamu na kuyatolea maamuzi.

**C. Mhimili wa Mahakama**

Mahakama ni chombo kikuu cha utoaji haki nchini Tanzania, ambapo kuna mahakama kadhaa ambazo zinatofautiana kimamlaka. Mahakama ya juu kabisa ni Mahakama ya Rufani, ambayo ina Majaji wa Mahakama ya Rufani, ambao husimamia na kutolea maamuzi kesi zote za rufaa. Ya pili ni Mahakama Kuu, ambayo pia ina majaji (Majaji wa Mahakama Kuu), ambao husimamia kesi zote katika ngazi hiyo na kuzitolea maamuzi. Mahakama zinazofuatia ni Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo – ambayo ndiyo mahakama ya chini kabisa. Tofauti na Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu, mahakama hizi za chini zina mahakimu. Mahakama Kuu ina vitengo mbalimbali, ikiwemo cha ardhi, biashara, kazi, na cha rushwa – ambacho kiliundwa mwaka 2016. Majaji wanateuliwa na Rais baada ya kupata ushauri wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, huku mahakimu wakichaguliwa na Tume hiyo moja kwa moja. Pia kuna Mahakama Maalum ya Katiba, ambayo ina mamlaka ya kushughulikia kesi za kikatiba, ikiwemo haki za binadamu. Ukiacha mahakama hizi, kuna mahakama za kijeshi-ambazo ni mahsusi kwa ajili ya wanajeshi.

Mahakama ya Rufani ni mahakama yenye mamlaka hadi Zanzibar, ambayo pia ina mahakama zake ziitwazo Mahamaka Kuu ya Zanzibar, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo. Pia kuna Mahakama ya Rufani ya Kadhi na Mahakama ya Kadhi.

***Wajibu katika ulinzi wa haki za binadamu:*** Mhimili huu una wajibu mkubwa katika ulinzi wa haki za binadamu, ikiwemo kutafsiri sheria mbalimbali, ikiwemo zinazohusu haki za binadamu; kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watuhumiwa wa vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu; na kusikiliza madai yanayohusiana na haki za binadamu. Mhimili huu pia hufanya mapitio ya maamuzi na vitendo vya watu na mamlaka mbalimbali kulingana na viwango vya haki za binadamu; huimarisha upatikanaji wa haki; hukuza utaratibu wa kisheria; na hutunga au kufanunua sheria kupitia kesi.



# 02

SURA YA PILI:

## HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA

# SURA YA PILI:
# HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA

## Utangulizi

Sura hii inajadili hali ya haki za kiraia na kisiasa Tanzania Bara kwa mwaka 2022, ikiangalia ukiukwaji wa haki hizo, masuala mbalimbali yaliyojitokeza, na mambo chanya yaliyofanyika. Sura hii imejikita katika haki ya kuishi, uhuru wa kujieleza, haki ya usawa mbele ya sheria na nafuu ya kisheria, haki ya kuwa huru na salama, uhuru wa kukusanyika, uhuru wa kujumuika, uhuru dhidi ya ukatili, haki ya kushiriki katika utawala, uhuru dhidi ya utesaji, na haki ya faragha. Haki hizi zimelindwa katika mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu, ikiwemo Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) wa mwaka 1966 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981. Hali kadhalika, zimelindwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Kwa mwaka 2022, hali ya haki za kiraia na kisiasa iliimarika kiasi ukilinganisha na mwaka 2021. Hii ilichangiwa na masuala mbalimbali chanya yaliyojitokeza ,ikiwemo kuimarika kwa hali ya uhuru wa vyombo vya habari, mpango wa Serikali wa kuondoa katazo la mikutano ya hadhara ya kisiasa, na mipango na hatua za Serikali kuanza kufanya maboresho ya haki jinai.


### 2.1. Haki ya Kuishi

Kwa mwaka 2022, masuala makuu yaliyoathiri haki ya kuishi Tanzania Bara ni pamoja na mauaji yanayotokana na kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, mauaji yanayotokana na maafisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi, adhabu ya kifo, na mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza.

#### *Mauaji yanayotokana na Wananchi Kujichukulia Sheria Mkononi*

Mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi yaliendelea kuwa mojawapo ya masuala makuu yanayoathiri haki ya kuishi. Mauaji haya

yamekuwa yakitokea zaidi Tanzania Bara, ambapo zaidi ya asilimia 95 ya matukio huripotiwa. Kwa mwaka 2022, LHRC ilikusanya matukio takribani 40 ya aina hii ya mauaji kupitia utafiti wa taarifa za vyombo vya habari na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu, ambayo ni matukio 18 zaidi ya yale yaliyokusanywa mwaka 2021. Hata hivyo, matukio haya huwa ni sawa na asilimia ndogo tu ya matukio ambayo huripotiwa polisi.





*# Mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi, 2015 to 2021*
*Chanzo: Takwimu za Jeshi la Polisi*

**Mtazamo & Wito wa LHRC:** Tabia ya wananchi kujichukulia sheria mkononi inaendelea kuwa changamoto katika jamii, na inaonekana kuchowewa zaidi na wananchi kutokuwa na imani na na mfumo wa haki jinai, hasa sababu ya hofu ya rushwa katika mfumo huo na kutokuwa na uelewa mzuri kuhusu sheria za jinai, ikiwemo suala la dhamana. Katika muktadha huu, ni muhimu kufanya maboresho ya mfumo wa haki jinai ili kurudisha imani ya wananchi. Lakini pia bado kuna haja ya wadau mbalimbali kuendelea kueneza uelewa kuhusu haki jinai na haki za mtuhumiwa ili kusaidia kuondoa baadhi ya mitazamo hasi miongoni mwa wanajamii. Wananchi pia wanahimizwa kutojihusisha na vitendo vya kujichukulia sheria mkononi na kuacha mkondo wa sheria ufanye kazi yake. Kadhalika, kuna haja ya kueneza uelewa kuhusu sheria na kanuni mbalimbali zinazohusiana na haki jinai, pamoja na madhara au athari zinazotokea sababu ya wananchi kujichukulia sheria mkononi.

### *Mauaji yanayotokana na maafisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi na ukatili unaofanywa dhidi ya maafisa wa vyombo hivyo*

Kwa mwaka 2022, LHRC ilikusanya matukio kumi ya mauaji yanayotokana na maafisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi, ambayo ni tukio moja zaidi ukilinganisha na matukio yaliyokusanywa mwaka 2021. Matukio haya yaliripotiwa katika Mikoa ya Kigoma, Mtwara, Kilimanjaro, Morogoro, Tabora, na Lindi, yakifanywa na askari sungusungu, askari wanyamapori, na askari polisi. Matukio kama haya ya maafisa wa

vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi na kusababisha mauaji pamoja na matukio mengine ya ukiukwaji wa miiko ya kazi yanayofanywa na maafisa hao yanaonyesha ni kwa kiasi gani kuna haja ya kuanzishwa chombo huru cha kiraia cha kuangalia utendaji kazi wa maafisa wa vyombo vya dola, ambacho kitasaidia kurejesha au kuongeza imani ya umma kwenye vyombo hivyo, kuongeza uadilifu miongoni mwa maafisa wa vyombo vya dola, na kuongeza uwajibikaji.




*# Matukio ya mauaji yanayotokana na maafisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi yaliyokusanywa na LHRC kuanzia mwaka 2016 hadi 2022*

**Wito wa LHRC:** Maafisa wa vyombo vya dola, wakiwemo askari polisi, kutojihusisha na vitendo vya matumizi ya nguvu kupita kiasi na kinyume na sheria ambayo yanapelekea kutokea kwa vifo vya watuhumiwa wa uhalifu ili kukidhi matakwa ya viwango vya kitaifa na kimataifa, ikiwemo Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi (PGO) na Kanuni za Umoja wa Mataifa za Utendaji Kazi wa Maafisa wa Vyombo vya Dola. Kuna haja pia ya kuundwa kwa chombo maalum cha kuchunguza utendaji kazi wa maafisa wa vyombo vya dola, ikiwemo askari polisi, ambacho mojawapo ya kazi zake itakuwa ni kuchunguza tuhuma za mauaji yanayotokana na maafisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi.

**Haja ya kuwa na chombo huru cha kuangalia utendaji wa maafisa wa vyombo vya dola**

Kuna sababu nzuri kadhaa za kuanzishwa kwa chombo huru cha kuangalia utendaji wa maafisa wa vyombo vya dola, ikiwemo:

- **Kurejesha au kuongeza imani ya umma:** Hii ni muhimu kwa ajili ya wanajamii kuona kwamba maafisa wa vyombo vya dola wanawajibishwa kwa matendo yao kwa njia ya uwazi.
- **Kanuni za haki asilia:** Kwa mujibu wa kanuni hii, mtu hawezi kuwa hakimu au jaji kwenye kesi yake mwenyewe (kanuni dhidi ya upendeleo).
- **Kuzuia ukiukwaji wa miiko na utamaduni wa kutochukuliwa hatua:** Chombo huru kitakuwa jicho la pili kwa vyombo vya ndani vya uchunguzi, na pia wanajamii watakuwa huru zaidi kutoa malalamiko yao dhidi ya maafisa kwenye chombo hicho kuliko kituo cha polisi.
- **Hofu:** Wanajamii wanaweza kusita kupeleka malalamiko kuhusu askari polisi kwa polisi wenyewe kwa sababu ya hofu.

- **Fursa ya kujifunza:** Uwepo wa chombo huru cha kuangalia utendaji wa maafisa wa vyombo vya dola unatoa fursa kwa vyombo hivyo kujifunza na kuona namna bora ya kuboresha huduma.
- **Kuisaida mifumo ya ndani ya uchunguzi:** Chombo huru kinaweza kuisaidia mifumo ya ndani ya uchunguzi kwa kuwa pia kinaweza kuaminika zaidi kwenye macho ya watu na kutofanya upendeleo wowote. Pia, ni rahisi zaidi kwa watu kupata taarifa kuhusu matokeo ya uchunguzi wa chombo hicho.

Kwa upande mwingine, mwaka 2022 LHRC ilikusanya matukio nane (8) ya mashambulizi dhidi ya maafisa wa vyombo vya dola, ambapo maafisa saba (wote wa kiume) waliuwawa na mmoja kujeruhiwa vibaya. LHRC inakemea vikali vitendo vya wananchi kuwashambulia na kuwafanyia vitendo vya ukatili maafisa wa vyombo hivi.

**Wito wa LHRC:** Wananchi kutojihusisha na vitendo vya kuwashambulia maafisa wa vyombo vya dola, kwani kufanya hivyo siyo tu ni kosa kisheria, bali pia ni ukiukwaji wa haki za maafisa hao kama binadamu. Pia, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ishirikiane na wadau wengine kueneza uelewa kuhusu suala hili kama njia ya kuzuia vitendo vya ukatili dhidi ya maafisa wa vyombo vya dola.

### *Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino*

Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, hasa ya watu wanaosadikiwa kuwa wachawi, yaliendelea kuwa tatizo katika sehemu mbalimbali Tanzania Bara. Kwa mwaka 2022, LHRC ilikusanya matukio 17 ya mauaji hayo, yaliyoripotiwa katika Mikoa ya Morogoro, Shinyanga, Mwanza, Kilimanjaro, Tabora, na Njombe. Matukio haya ni matukio 19 pungufu ya yale yaliyoripotiwa mwaka 2021. Wahanga wengi (asilimia 52) walikuwa ni wanawake na mmojawapo wa wahanga alikuwa ni mtu mwenye ualbino. Waganga wa kienyeji walidaiwa kuchochea mauaji hayo kwa kiasi kikubwa.




*# Matukio ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina – 2017 hadi 2021*
*Chanzo: Takwimu za Jeshi la Polisi*


LHRC pia imebaini kwamba mashambulizi na mauaji ya watu wenye ualbino yameanza kuibuka upya katika miaka ya hivi karibuni.

Mathalani mwaka 2021 kulikuwa na tukio la mauaji ya kutisha ya mtoto mwenye ualbino mkoani Tabora, na mwaka 2022 mtu mwenye ualbino, Joseph Mathias (50), mkazi wa Mwanza, alishambuliwa na kukatwa mkono, jambo lililopelekea avuje damu nyingi na hatimaye kufariki. Hali hii siyo nzuri na inaonyesha hitaji la hatua za haraka na makusudi kuwalinda watu wenye ualbino.

**Wito wa LHRC:** Kiundwe kikosi kazi maalum, ambacho kitajumuisha wawakilishi kutoka Jeshi la Polisi Tanzania, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na asasi za kiraia, kwa ajili ya kuchuguza mashambulizi na mauaji hayo na kuja mikakati ya muda mrefu ya kuwalinda watu wenye ualbino.

### *Adhabu ya kifo*

Adhabu ya kifo, ambayo imekuwa ikipingwa kwa kukiuka haki ya kuishi na kuwa adhabu ya kikatili, iliendelea kutolewa na mahakama mwaka 2022 kwa mujibu wa sheria. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020 hadi 2022, LHRC imekusanya jumla ya adhabu 98, ambapo 91 (asilimia 93) zilitolewa kwa wanaume na 7 (asilimia 7) zilitolewa kwa wanawake. Kwa mwaka 2022 pekee, LHRC ilikusanya adhabu 44, zikiongezeka kutoka adhabu 24 mwaka 2021. Kati ya adhabu hizo 44, adhabu 41 zilitolewa kwa wanaume na 3 zilitolewa kwa wanawake. Kwa upande mwingine, nchi mbalimbali duniani ziliendelea kuungana katika mapambano ya kuondoa adhabu ya kifo mwaka 2022, ambapo nchi 125 zilipiga kura ya kuunga mkono Azimio la Baraza la Umoja wa Mataifa kuhusu kusitisha adhabu ya kifo. Kwa upande wa nchi zinazofanya mabadiliko ya kisheria kuhusu adhabu ya kifo, mwaka 2022 nchi tatu zaidi za Kiafrika, ambazo ni Afrika ya Kati, Guinea ya Ikweta, na Zambia, pia zilifanya marekebisho ya kisheria kuondoa adhabu ya kifo katika sheria. Pia, katika kesi ya *Marthine Christian @ Msuguri dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,* Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ilisema kwamba adhabu ya lazima ya kifo inakiuka haki ya kuishi.





*# Adhabu za kifo zilizokusanywa na LHRC – 2017 had 2022*
*Chanzo: LHRC, 2022*

| Sababu za Kupinga Adhabu ya Kifo |
|---|
| • Adhabu ya kifo ni ya kikatili na isiyo ya kibinadamu, inayokiuka haki ya kuishi.. |
| • Watu wasio na hatia wamekuwa wahanga wa adhabu ya kifo katika sehemu mbalimbali duniani. |
| • Adhabu ya kifo hairekebishiki mara itakapotekelezwa! |
| • Zaidi ya asilimia 70 ya nchi zote duniani zimeondoa adhabu ya kifo katika sheria au mazoea. |
| • Adhabu ya kifo imeshindwa kuzuia vitendo vya uhalifu katika nchi nyingi duniani, ikiwemo Marekani. |
| • Adhabu ya kifungo cha maisha jela ni mbadala mzuri wa adhabu ya kifo. |
| • Mahakama katika nchi jirani kama vile Kenya , Malawi, na Uganda zimetamka kwamba adhabu ya kifo inakinzana na Katiba. |
| • Kupinga adhabu ya kifo hakumaanishi kutokuwa na huruma kwa wahanga wa mauaji. |
| • Jamii inayoheshimu maisha haiwezi kuuwa binadamu kwa makusudi. |
| • Mara nyingi adhabu ya kifo hutolewa kwa watu wa kipato cha chini au maskini ambao hawana uwezo wa kupata uwakilishi mzuri wa kisheria. |

**Wito wa LHRC:** Ikiwa ni miongoni mwa nchi ambazo hazitekelezi adhabu ya kifo, ipo haja ya Tanzania kujiunga na nchi nyingine nyingi duniani na kuchukua hatua ya kuondoa kabisa adhabu ya kifo. Kwa sasa, ni nchi 53 pekee ambazo zinaendelea kuwa na adhabu ya kifo na kutekeleza adhabu hiyo, huku nchi 29 zikiwa hazitekelezi adhabu hiyo, ikiwemo Tanzania. Nchi jirani kama vile Rwanda, Malawi, na Msumbiji ni miongoni mwa nchi 112 duniani ambazo zimeondoa adhabu ya kifo, hivyo Tanzania nayo inaweza kuchukua hatua zaidi na kuwa miongoni mwa nchi hizo.

### *Mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza*

Mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza yaliendelea kuwa kikwazo kwa haki ya kuishi mwaka 2022. LHRC ilikusanya matukio 33, ambayo ni 2 pungufu ya yale yaliripotiwa na kukusanywa mwaka 2021. Matukio hayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Geita, Dodoma, Lindi, Mbeya, Singida, Mwanza, Shinyanga, Katavi, Mtwara, Dar es Salaam, Ruvuma, Mara, Morogoro, Rukwa, Songwe, na Manyara. Kati ya wahanga hao 33, wahanga 31 walikuwa wanawake na 2 walikuwa wanaume. Asilimia 52 ya matukio yalisemekana kusababishwa na wivu wa kimapenzi.




*Mgawanyo wa matukio ya mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2022 kwa kanda*

Kwa upande wa mgawanyo wa matukio kimkoa, Mkoa wa Mtwara ulikuwa na matukio mengi ziaidi (6), ukifuatiwa na Dar es Salaam (4), Shinyanga (3), Dodoma (3), Katavi (3), na Mwanza (2).

**Mtazamo wa LHRC:** Ukatili dhidi ya mwenza na mauaji yanayofanywa na mwenza dhidi ya mwenza ni tishio kubwa kwa haki ya kuishi, haki ya afya, haki ya kuwa huru na salama, na uhuru dhidi ya ukatili. Idadi ya matukio yanayoripitiwa inaleta wasiwasi na kuna uwezekano mkubwa kwamba kuna matukio mengine mengine hayaripotiwi. Pia, LHRC imebaini kwamba matukio ya aina hii yanatokea zaidi miongoni mwa makundi ya vijana na watu wazima.

**Wito wa LHRC:** Kuna haja ya wadau wote kuunganisha nguvu pamoja na kutengeneza mikakati ya kuwalinda wanawake dhidi ya ukatili dhidi ya mwenza na/au ukatili majumbani, kwa kuwa ndiyo wamekuwa wahanga zaidi. Sehemu nzuri ya kuanzia ni utungaji wa sheria ya ukatili wa kijinsia au ukatili majumbani ili kuwalinda wenza, kwa kuwa imeshafahamika kwamba matukio mengi ya ukatili wa kijinsia hutokea nyumbani.

### *Matukio ya watu kupotea*

Mwaka 2022 hakukuwa na taarifa zozote mpya zilizotolewa kuhusu upoteaji wa watu kadhaa katika miaka ya nyuma, ikiwemo Azory Gwanda, ambaye alipotea katika mazingira ya kutatanisha mkoani Pwani mwezi Novemba 2017; Ben Saanane, mwanaharakati wa kisiasa, ambaye alipotea mwaka 2016; na Simon Kanguye, aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, aliyepotea mwaka 2017.

**Wito wa LHRC:** Serikali na Jeshi la Polisi Tanzania kuongeza kasi ya chunguzi wa matukio ya watu kupotea na kutoa mrejesho wa mara kwa mara kwa umma na wanafamilia, sambamba na kuwakamata watuhumiwa. Utoaji wa mrejesho ni muhimu pia kwa familia ili ziweze kujua nini kiliwapata ndugu zao na kuendelea na maisha yao.

### *Ajali za barabarani*

Ajali za barabarani ziliendelea kutokea sehemu mbalimbali nchini,nyingi zikisababishwa na uzembe kwa upande wa madereva wa vyombo vya moto. Mnamo mwezi Novemba 2022, Jeshi la Polisi liliripoti kwamba ajali za barabarani nchini Tanzania ziliongezeka kwa asilimia 0.8 katika kipindi cha Januari hadi Novemba 2022, ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2021. Ajali zilidaiwa kusababishwa na uendeshaji wa kasi kupita kiasi, ueandeshaji mbaya, na uendeshaji huku dereva kalewa.




*# Ajali za barabarani na vifo nchini Tanzania, 2020 hadi 2022*
*Chanzo: Takwimu za Jeshi la Polisi*

Katika ngazi ya familia, ajali za barabarani zimepoteza maisha ya watafuta mkate na wapendwa katika familia, zikiwaacha waume bila wake, wake bila waume, wazazi bila watoto, na watoto bila wazazi. Zinachangia kuvuruga umoja katika familia, kupunguza kipato, kutengeneza migogoro ya kifamilia, na kusababisha talaka au kuachana, huku wahanga wakiathirika kijamii, kisaikolojia, na kiuchumi. Wanawake na watoto wanaathirika zaidi na ajali za barabarani.

Katika ngazi za jamii na taifa, ajali za barabarani zinapoteza maisha ya wataalamu, wanataalauma, na wazalishaji, ambao wana mchango mkubwa katika uchumi na maendeleo. Katika nchi nyingi duniani, gharama za kiuchumi za ajali za barabarani zinaweza kufikia hadi asilimia 5 ya pato la taifa. Hivyo, ajali za barabarani zinaongeza gharama za matumizi kwa upande wa Serikali, ikiwemo katika sekta ya afya, ambayo inaelemewa na wahanga wa ajali za barabarani wanaohitaji kufanyiwa operesheni.

**Mtazamo wa LHRC:** Pamoja na jitihada mbalimbali zilizofanywa na Jeshi la Polisi, bado ajali za barabarani ni changamoto kubwa nchini Tanzania. Maisha mengi yamepotea sababu ya ajali hizo, na watu wengi kuachwa wakiwa na majeraha na ulemavu wa kudumu, jambo ambalo lina athari kubwa kwenye maendeleo ya kijamii na kitaifa. Ajali nyingi zinasababishwa na makosa ya kibinadamu (uzembe) kama vile kuendesha vibaya, kuendesha huku mtu kalewa, na kuvipita vyombo vingine vya moto bila umakini. LHRC imebaini pia kwamba ukosefu wa usingizi wa kutosha kwa

madereva wa mabasi ya mkoani na malori pia kunachangia ajali za barabarani, kwa sababu ya kupewa kazi nyingi na muda mchache, hivyo kukosa muda wa kupumzika, hali inayowafanya wakose umakini barabarani.

**Wito wa LHRC:** Jeshi la Polisi na wadau wengine, wakiwemo wakala wa barabara, kuongeza jitihada za kuhakikisha usalama barabarani na kuzuia ajali za barabarani, ikiwemo kupitia programu za kueneza uelewa, pamoja na kupambana na rushwa katika sekta ndogo ya usafirishaji wa kutumia barabara.

.

## 2.2. Uhuru wa Kujieleza

Kwa mwaka 2022, masuala makuu yaliyoathiri uhuru wa kujieleza kwa upande wa Tanzania Bara ni pamoja na uwepo sheria na kanuni zenye vifungu vinavyominya uhuru huo, nia ya Serikali ya kurekebisha baadhi ya sheria zinazohusiana na uhuru wa kujieleza, Serikali kuvifungulia vyombo vya habari vinne vilivyofungiwa miaka ya nyuma, na ukamataji na unyanyasaji wa wanahabari.

Sheria ambazo zina vifungu vinavyominya uhuru wa vyombo vya habari kinyume na viwango vya kimataifa vya uhuru huo ni pamoja na Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015, na Kanuni za Maudhui ya Mtandao za mwaka 2020, ambazo hadi kufikia tarehe 31 mwezi Desemba 2022 zilikuwa bado hazijarekebishwa. Hata hivyo, wadau waliendelea kutoa wito wa sheria na kanuni hizo kurekebishwa. Pia, kikosi kazi kilichoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan kukusanya maoni kuhusu demokrasia ya vyama vingi nchini kilitoa pendekezo la Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 kurekebishwa, na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mh. Nape Nnauye, alisema kwamba Serikali imeshaanza mchakato wa kurekebisha sheria hiyo pamoja na Sheria ya Upatikanaji Taarifa, pia ya mwaka 2016, pamoja na kanuni zake.

Mnamo mwezi Julai mwaka 2022, wadau mbalimbai wa habari walipendekeza kwamba ni vyema wanahabari wakaunda chombo chao wenyewe cha kuangalia na kusimamia utendaji kazi wao ili kupunguza uingiliaji wa Serikali kwenye masuala yao. Wadau hao pia walimsifia na kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari, ikiwemo kuvifungulia vyombo vya habari vya Tanzania Daima, Mawio, Mwanahalisi na Mseto, vilivyofungiwa mwaka 2016 na 2017.

Pamoja na uhuru wa vyombo vya habari kuonekana kuimarika kiasi, Tanzania

ilifanikiwa kupanda nafasi moja pekee katika Viwango vya Uhuru wa Vyombo Habari Duniani vya mwaka 2022, ambapo ilipanda kutoka nafasi ya 124 kati ya nchi 180 mwaka 2021 hadi nafasi ya 123 mwaka 2022. Matukio ya ukiukwaji wa uhuru wa vyombo vya habari pia yaliendelea kuripotiwa, ambapo LHRC ilikusanya matukio yapatayo 10.

**Wito wa LHRC:** Serikali na Bunge kuchukua hatua ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 kama ilivyoelekezwa katika hukumu ya Mahakama ya Haki ya Afrika Mashiriki kuhusu sheria hiyo ya mwezi Machi mwaka 2019, ili kuimarisha ulinzi wa uhuru wa kujieleza nchini. Pia, sheria nyingine zilizotajwa hapo juu zinazominya uhuru wa kujieleza zipitiwe na kufanyiwa marekebisho kulingana na viwango vya kimataifa vya uhuru wa kujieleza.

## 2.3. Uhuru wa Kujumuika na Kukusanyika

Masuala makuu yaliyoathiri ufurahiaji wa uhuru wa kujumuika na kukusanyika kwa upande wa Tanzania Bara ni pamoja na uwepo wa sheria na kanuni zenye vifungu vinavyominya uhuru huo, wito wa sheria na kanuni hizo kufanyiwa marekebisho, na katazo la mikutano ya hadhara ya kisiasa. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Vyama vya Kisiasa, ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2019, Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Msingi (BRADEA), ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2021, na Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali, ambazo bado hazijafanyiwa marekebisho illi kuendana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu. Pia, mwaka 2022 wadau mbalimbali na wajumbe wa kikosi kazi kilichoundwa na Rais kukusanya maoni kuhusu demokrasia ya vyama vingi walitoa mapendekezo ya kurekebishwa kwa Sheria ya Vyama vya Siasa na kuondolewa kwa katazo la mikutano ya hadhara ya kisiasa.

**Wito wa LHRC:** Serikali kuchukua hatua ya kufanya mapitio na marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Msingi (BRADEA), na Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali, ili ziendane na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

## 2.4. Haki za Usawa mbele ya Sheria na Nafuu ya Kisheria


Pamoja na juhudi na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali na Mhimili wa Mahakama kukuza na kulinda haki za usawa mbele ya sheria na nafuu ya kisheria, bado kuna changamoto kadhaa ambazo ziliendelea kuathiri utekelezaji madhubuti

wa haki hizi mwaka 2022.


Masuala muhimu yaliyoathiri haki za usawa mbele ya sheria na nafuu ya kisheria ni pamoja na: sheria zinazoathiri utekelezaji madhubuti wa haki ya usawa mbele ya sheria; vikwazo vya upatikanaji wa haki, ikiwemo upungufu wa watumishi wa kimahakama, ucheleweshaji katika chunguzi, na kesi kuchukua muda mrefu; na changamoto za haki jinai kama vile uwekaji kuzuizini wa mahabusu magerezani kwa muda mrefu, uchunguzi kuchukua muda mrefu na kesi kuahirishwa mara kwa mara, msongamano wa mahabusu magerezani na katika vituo vya polisi, changamoto za utaratibu wa kukiri kosa, na mtuhumiwa kutofikishwa mahamani ndani ya muda unaotakiwa kisheria.

## *Vikwazo vya Upatikanaji wa Haki*

Wanajamii walioshiriki katika utafiti wa haki za binadamu mwaka 2022 waliainisha vikwazo kadhaa vya ukapatikaji wa haki. Miongoni mwa vikwazo hivyo ni rushwa, ambayo ilitajwa kama kikwazo kikuu (asilimia 82), ikifuatiwa na urefu wa kesi au mashauri mahakamani (asilimia 54), uelewa mdogo kuhusu sheria (asilimia 54), gharama za uwakilishi mahakamani (asilimia 37), taratibu ndefu /ngumu za kisheria (asilimia 30), na umbali wa mahakama (asilimia 25).




*%Vikwazo vya ufikiaji haki*




*Mtazamo wa wanajamii kuhusu rushwa kama kikwazo cha upatikanaji wa haki*

> *'...Nilikua nina kesi mahakamani, lakini karani alivyokuwa ananiongelesha nikaona kabisa anataka rushwa,nikawa najifanya sielewi..kuna siku akaniambia kaka changamka utalala hapa.'*
>
> **Mwanajamii, Manyoni – Singida**

Wadau na wanajamii mbalimbali katika mikoa iliyotembelewa pia walielezea ucheleweshaji katika chunguzi na usikilizaji wa kesi na uahirishaji wa kesi wa mara kwa

mara kama vikwazo vikubwa vya upatikanaji wa haki.


> *Kesi zinaahirishwa bila sababu za msingi, kesi inapigwa tarehe kila siku...mtu unapoteza pesa kusafiri kila mara kwenda kwenye kesi alafu ukifika unaambiwa kesi imehairishwa mpaka tarehe flani,ukienda tena majibu ni hayohayo.'*
> **Mwanajamii, Halmashauri Wilaya Singida – Singida**

Changamoto nyingine ya upatikanaji wa haki iliyotajwa katika mikoa iliyotembelewa, ikiwemo Mbeya, Njombe, Kagera, na Katavi, ni kutokuwepo kwa vituo vya polisi katika baadhi ya maeneno. Pia, kuna wanajamii walililamika kuhusu upatikanaji hafifu wa msaada wa kisheria, ikiwemo katika wilaya ambazo zina watoa huduma za msaada wa kisheria. Jambo hili liliibuliwa katika mikoa 14 kati ya 20 iliyotembelewa (asilimia 70), ikiwemo Kigoma, Geita, Katavi, Kilimanjaro, na Mbeya. Kutokuwa na fedha za kuendesha ofisi kulitajwa kama mojawapo ya changamoto.

> *'...ofisi nyingi za msaada wa kisheria za huku Katavi zimefungwa kutokana na hakuna hela hivyo kila mtu anatafuta kazi nyingine kutokana na pesa ya kuendesha ofisi hakuna..hivyo jamii inakosa huduma kutokana na uchache wa ofisi za msaada wa kisheria"*
> **Mkurugenzi wa Tanganyika Pamoja Tuzungumze – Tanganyika, Katavi**

**Wito wa LHRC:** Asasi za kiraia na watoa huduma wengine wa msaada wa kisheria kuelekeza afua za utoaji wa msaada wa kisheria katika maeneo ya vijijini zaidi na kufanya jitihada za makusudi kuwafikia wanawake wanaoishi vijijini.

Kwa upande wa imani na taasisi za utoaji haki na utatuzi wa migogoro, viongozi wa kidini walionekana kuaminika zaidi na wanajamii (asilimia 70), wakifuatiwa na kikao cha familia (asilimia 60), mashirika yasiyo ya kiserikali/watoa huduma za kisheria (asilimia 59), na mwenyekiti wa Kijiji (asilimia 41). Taasisi nyingine ni viongozi wa kitamaduni (asilimia 39), mahakama (asilmia 38), baraza la kata (asilimia 29), na polisi (asilimia 19).




*% Mitazamo ya wanajamii kuhusu imani kwenye taasisi za utoaji haki na utatuzi wa migogoro*

Pamoja na changamoto mbalimbali zinazoukabili mfumo rasmi wa haki, zaidi

kidogo ya nusu ya wanajamii (asilimia 57), walisema kwamba wanapendelea zaidi kutafuta haki kupitia mfumo huo, ikiwemo kupitia mahakama na mabaraza.

### *Masuala na changamoto katika haki jinai*

Kwa mwaka 2022, wadau mbalimbali wa kiserikali na wasio wa kiserikali, akiwemo Mh. Rais Samia Suluhu Hassan, waliendelea kutoa wito wa kufanyika kwa maboresho katika mfumo wa haki jinai nchini. Mnano mwezi Julai 2022, Rais aliunda kamati ya watu 12, ikiongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Mh. Mohamed Othman Chande, ili kuchunguza utendaji kazi wa taasisi za haki jinai.

Ripoti maalumu ya uchunguzi ya hivi karibuni ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu mfumo wa haki jinai, imeonyesha kwamba mojawapo ya sababu za ucheleweshaji katika uchunguzi wa polisi ni kutozingatia muda wa kufanya uchunguzi uliowekwa katika Kanuni za Jeshi la Polisi za mwaka 2021, ambao ni mwaka mmoja kwa makosa makubwa na miezi sita kwa makosa mengine. Sababu nyingine ni pamoja na polisi kuchelewa kupata matokeo ya uchunguzi wa kisayansi kutoka kwa wataalamu, jiografia ya eneo la tukio, pale ambapo uhalifu umefanyika katika maeneo ya pembezoni; kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa rasilimali watu kusaidia uchunguzi; na kutokuwepo kwa rasilimali za kutosha katika ufanyaji wa uchunguzi.

Changamoto nyingine kuu katika haki jinai

| ***Maelekezo ya Rais Samia kuhusu maboresho ya haki jinai*** Tangu aingie madarakani, Rais Samia amekuwa mstari wa mbele kutaka mabadiliko ya mfumo wa haki jinai ili kutatua changamoto mbalimbali, ikiwemo uwekaji kizuizini wa wahabusu kwa muda mrefu, ubambikaji wa kesi, rushwa, na ucheleweshaji katika uchunguzi na ukamilishaji wa kesi. Ametoa maelekezo mbalimbali ya kuboresha haki jinai, ikiwemo kwa Jeshi la Polisi na Mhimili wa Mahakama. LHRC inampongeza Rais kwa utashi wake wa kisiasa katika suala hili la msingi kwa haki za binadamu. Sambamba na hilo, LHRC inatoa wito kwa Serikali kuendelea kuchukua hatua za kuboresha mfumo wa haki jinai ili kulinda haki za binadamu, ikiwemo kufanya maboresho ya sheria na sera zinazohusika na mfumo huo. | ***Utambuzi wa LHRC***  |
|---|---|

ambazo zimeibuliwa katika ripoti ya CAG ni pamoja na uwezo usiotelesheza wa kufanya uchunguzi wa jinai; uahirishaji wa kesi mara kwa mara, ambao unasababishwa zaidi na kutokamilika kwa uchunguzi kwa wakati (asilimia 60); ucheleweshaji katika ukamilishaji wa kesi; usimamizi usioridhisha wa mafaili ya kesi wakati wa uchunguzi na kutokuwepo kwa muda maalum wa kukamilisha mashtaka; upungufu wa mawakili wa serikali katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; na mianya katika ufuatiliaji na tathmini ya utendaji kazi wa vyombo vya utoaji haki pamoja na uratibu wa vyombo hivyo, kwa upande wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Uwekaji kizuizini wa watuhumiwa/mahabasu kwa muda mrefu pia uliendelea kuwa changamoto katika haki jinai, hivyo kukiuka haki ya kesi kuendeshwa kwa haki na kanuni ya mtuhumiwa kutokuwa na hatia hadi pale ambapo mahakama itasema vinginevyo. Tatizo hili linachangiwa na changamoto ya uahirishaji wa kesi mara kwa mara. Ripoti maalumu ya uchunguzi wa haki jinai ya CAG iliangalia pia suala hili la uahirishaji wa kesi katika ngazi tofauti za mahakama katika mikoa mbalimbali. Matokeo yalionyesha kwamba kiwango cha juu cha uahirishaji wa kesi kilitokea katika Mahakama ya Hakimu Mkazi, ambapo wastani wa kesi kuahirishwa ulikuwa ni mara 68, ikifuatiwa na Mahakama ya Wilaya, ambapo wastani ulikuwa ni mara 48, na Mahakama Kuu mara 31. Kwa kesi moja moja, kiwango cha juu zaidi cha uahirishaji wa kesi kilionekana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma, ambapo kuna kesi iliahirishwa mara 101 kabla ya usikilizaji wake kukamilika. Sababu kubwa ya uahirishwaji wa kesi ilikuwa ni uchunguzi kutokamilika.




*Sababu za kesi kuahirishwa katika mahakama nchini Tanzania*
*Chanzo: Ripoti ya CAG ya Haki Jinai 2022*

Changamoto za kitehama pia ziliendelea kuathiri usimamizi wa haki jinai, ikiwemo changamoto ya mioundumbinu katika mahakama na magereza, na kutopatikana kwa wavuti (internet) thabiti. Changamoto hizi zinaweza kusababisha athari kubwa kwa watuhumiwa.

**Wito wa LHRC:** Serikali kufanya maboresho yanayohitajika katika mfumo wa haki jinai

ili kuondoa adha kama vile kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu kabla ya kesi kuanza kusikilizwa na kupunguza matumizi ya utaratibu wa uwekaji kuzuizini wa watuhumiwa. Pia, ili kulinda haki za watuhumiwa, hasa wahanga wa ubambikaji kesi, Serikali haina budi kuhakikisha uzingatiaji wa ukomo wa muda wa kumuweka mtu kuzuizini, ikiwemo kwa makosa makubwa, na kuhakikisha kwamba kesi zinafunguliwa baada ya uchunguzi kukamillika na si kabla. Pia, sheria ielezee wazi ni nani anatakiwa kuhakikisha ukomo wa muda unazingatiwa na kuelezea taratibu za kufuatwa pale ambapo hili halijazingatiwa.

## 2.5.Haki ya kuwa Huru na Salama

Kwa mwaka 2022, masuala makuu yaliyoathiri haki ya kuwa huru na salama kwa upande wa Tanzania Bara ni pamoja na ukamataji na uwekaji kizuizini kinyume na sheria; kunyimwa dhamana; ubambajikaji wa kesi; kukosekana kwa vituo vya polisi katika baadhi ya kata; wasiwasi kuhusiana na usalama wa raia kufuatia matukio ya mauaji na mashambulizi; ucheleweshaji katika kufanya na kukamilisha uchunguzi; na ulinzi na usalama mitandaoni.

### *Ukamataji na uwekaji kizuizini kinyume na sheria*

Ukamataji na uwekaji kizuizini kinyume na sheria huwakosesha watu uhuru wao. Kwa mwaka 2022, LHRC ilikusanya matukio takribani kumi na mbili ya ukamataji na uwekaji kizuizini wa watu kinyume na sheria kupitia programu yake ya ufuatiliaji wa haki za binadamu, utafiti wa taarifa za vyombo vya habari, na utafiti wa haki za binadamu uliofanyika katika mikoa mbalimbali. Matukio haya ni ongezeko la matukio manne ukilinganisha na matukio yaliyokusanywa mwaka 2021. Miongoni mwa wahanga walikuwa ni waandishi wa habari sita na mwanachama mmoja wa chama cha upinzani cha kisiasa.

### *Upungufu wa vituo vya polisi*

Kukosekana kwa vituo vya polisi katika baadhi ya kata kulijatajwa pia kama changamoto katika ufurahiaji na utekelezaji wa haki ya kuwa huru na salama. Mnamo mwezi Aprili 2022, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mh. Hamad Yusuf Masauni, alisema kwamba Tanzania inakabiliwa na upungufu wa vituo vya polisi (Daraja B) 470. Baadhi ya wakazi wa Kata ya Mtapenda wilayani Nsimbo mkoani Katavi walioshiriki katika utafiti pia walilalamika kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu katika kata yao kwa sababu ya kutokuwepo kwa kituo cha polisi.

### *Wimbi la mauaji na mashambulizi*

Wimbi la mauaji na mashambulizi, ikiwemo

mashambulizi yaliyofanywa na vikundi vya vijana vya kihalifu maarufu kama 'Panya Road' jijni Dar es Salaam, 'Panya Kaloa' jijini Dodoma and 'Panya Teleza' mkoani Pwani, yalikuwa pia tishio kwa haki ya kuwa salama. Vikundi hivyo vya kihalifu, ambavyo vilipendelea kutumia mapanga, vilisababisha mtafaruku katika maeneo mbalimbali katika mikoa hiyo, kwa kuwavamia watu nyumbani kwao, kuwashambulia, na kuiba vitu mbalimbali. Polisi waliripoti kuwakamata zaidi ya vijana 150 wa kikundi cha 'Panya Road.' Kabla ya matukio haya ya vikundi vya kihalifu vya vijana, nchi ilishtushwa na mauaji yaliyotokea katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara mwanzoni mwa mwaka, Januari 2022. Katika mwezi huu pekee, LHRC ilikusanya matukio takribani 20 ya watu kuuwawa, ikiwemo mauaji ya kikatili ya wanawake watatu mkoani Mwanza baada ya kubakwa. Mnamo tarehe 1 Februari mwaka huu, Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilitangaza kwamba imeunda kamati maalum ya kuchunguza wimbi la mauaji yaliyotokea nchini na kuleta majibu ndani ya siku 21. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Disemba 2022, LHRC ilikuwa haijasikia lolote kuhusu ripoti hiyo.

### *Ubambikaji kesi na ucheleweshaji katika chunguzi*

Viongozi mbalimbali wa Serikali, akiwemo Rais, waliendelea kuongelea changamoto za ubambikaji kesi na ucheleweshaji katika ufanyaji wa uchunguzi mwaka 2022. Mathalani, mnamo mwezi Novemba 2022, Rais Samia Suluhu Hassan alisema kwamba mahabusu wengi waliopo magerezani ni wahanga wa ubambakaji kesi. Kabla ya hapo, mnamo mwezi Agosti 2022, Jeshi la Polisi Tanzania lilitangaza kwamba jumla ya kesi za kubambika 1,844 zilifutwa mahakamani ili kupunguza msongamano magerezani. Ripoti ya miaka 20 ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, iliyotolewa na tume hiyo mwezi Septemba 2022, pia ilionyesha kwamba ubambikaji kesi na ucheleweshaji katika ufanyaji uchunguzi ni mojawapo ya changamoto kubwa katika mfumo wa haki jinai nchini Tanzania.

### *Usafirishaji haramu wa binadamu*

Kwa mwaka 2022, usafirishaji haramu wa binadamu uliendelea kuwa tishio kwa haki ya kuwa huru na salama. Mnamo mwezi Aprili 2022, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mh. Hamad Yussuf Masauni, alisema kwamba wizara yake iliwaokoa jumla ya wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu 182 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, ambapo 171 kati yao waliokolewa nchini Tanzania na 11 nchini Iraq na Kenya. Kupitia utafiti wa taarifa za vyombo vya habari na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu,

LHRC ilikusanya matukio kumi na mbili ya usafirishaji haramu wa binadamu, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Mbeya, Singida, Dar es Salaam, na Dodoma. Matukio haya ni matukio nane pungufu ya yale yaliyokusanywa mwaka 2021. Hata hivyo, LHRC ilikusanya matukio mengine 83 kupitia utafiti wa haki za binadamu, yaliyoripotiwa katika mikoa kama vile Kigoma, Dodoma, Rukwa, Mbeya, Katavi, Morogoro, na Dar es Salaam.

Kwa upande mwingine, Serikali ilipongezwa kwa kupiga hatua katika mapambano dhidi ya usafirishaji haramu wa binadamu, ikiwemo kupitisha Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa 2021-2024 na kufanya marekebisho kadhaa kwenye Sheria ya Kupinga Usafirishaji Haramu wa Binadamu ya mwaka 2008. Hali kadhalika, mnamo mwezi Julai 2022, Waziri wa Katiba na Sheria, Mh. Damas Ndumbaro, alizindua Kikosi Kazi cha Ulinzi wa Mtoto dhidi ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu.

**Wito wa LHRC:** Serikali, hususan kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kushirikiana na wadau wengine katika kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya usafirishaji haramu wa binadamu, hasa katika mikoa ambayo usafirishaji haramu wa watoto huripotiwa zaidi kama vile Dodoma, Iringa, Mbeya, Manyara, Singida, Kilimanjaro, na Tanga.

### *Usalama na ulinzi mtandaoni*

Utafiti wa haki za binadamu uliofanyika katika mikoa 20 ya Tanzania Bara uliangazia pia suala la ulinzi na usalama mtandaoni. Utafiti huo ulibaini kwamba uelewa kuhusu usalama na ulinzi mtandaoni miongoni mwa wanajamii ni mdogo. Ni asilimia 15 ya washiriki wa utafiti pekee ndiyo walisema wana uelewa mkubwa sana au uelewa mkubwa kuhusu usalama na ulinzi mtandaoni na asilimia 10 pekee walisema wana uelewa mkubwa sana au uelewa mkubwa kuhusu sheria za usalama na ulinzi mtandaoni. Walipoulizwa kuhusu aina kuu za mashambulio mtandaoni, wengi wao (asilimia 46), walitaja wizi wa fedha, ukifuatiwa na matusi (asilimia 22), uonevu mtandaoni (asilimia 19), na wizi wa taarifa/utamblisho (asilimia 7). Karibia nusu ya washiriki (asilimia 44) pia walidai kwamba uonevu mtandaoni ni tatizo kubwa katika jamii, hasa katika maeneo ya mijini.

- Wanawake na watoto wapo katika hatari zaidi ya kufanyiwa shambulio mtandaoni, hasa ukatili wa mtandaoni na wizi wa taarifa au utambulisho.
- Asilimia 45 ya washiriki wa utafiti walisema kwamba wanatumia mwaka wa kuzaliwa au umri katika nywila (passwords)

zao, suala ambalo linawaweka katika hatari ya kushambuliwa na wavamizi wa kimtandao, wakati asilimia 46 walisema kwamba wanatumia nywila moja katika akaunti kadhaa tofauti, hasa vijana (asilimia 70). Sababu kuu ya kufanya hivyo ni urahisi wa kukumbuka nywila. Mkoani Mtwara, utafiti ulibaini kwamba kuna watu huwa wanawaomba watu wasiowahafamu vizuri, ikiwemo wafanyakazi katika maduka ya vifaa vya shule na ofisi (stationery) ili wasaidiwe kufungua akaunti za barua pepe, kufungua akaunti katika mitandao ya kijamii, na kutengeneza nywila za akaunti hizo, suala ambalo linahatarisha usalama na ulinzi wao mtandaoni.

**Wito wa LHRC:** Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknkolojia ya Habari, na Tume ya Haki za Binadam na Utawala Bora, kueneza uelewa wa umma kuhusu usalama na ulinzi mtandaoni.

## 2.6. Haki ya Kushiriki katika Utawala

Masuala makuu yaliyoathiri haki ya kushiriki katika utawala Tanzania Bara mwaka 2022 ni pamoja na vikwazo vya kisheria; wito wa kuboresha demokrasia ya vyama vingi; na haki ya wafungwa na mahabusu ya kupiga kura.

Katika kipindi cha miaka mingi huko nyuma, Serikali imechukua hatua kadhaa za kisheria na kitaasisi kuongeza na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika siasa. Hata hivyo, bado kuna vikwazo kadhaa ambavyo vinazuia utekelezaji madhubuti wa haki za kugombea nafasi za uongozi na kushiriki katika siasa. Vikwazo hivi vimeonekana katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na sheria za uchaguzi, ikiwemo Sheria ya Vyama vya Siasa iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019. Mathalani, Katiba haitambui wagombea binafsi, na inakataza matokeo ya urais kuhojiwa au kupingwa mahakamani. Hali kadhalika, marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa yameathiri zaidi haki ya kushiriki katika siasa, hasa kwa kumpatia Msajili wa Vyama vya Siasa mamlaka makubwa ambayo yanaingilia uhuru wa vyama vya siasa. Kwa upande wa wanawake, ushiriki usioridhisha katika siasa na uongozi unachangiwa kwa kiasi kikubwa na sheria ambazo hazijazingatia suala la jinsia, jambo linalofanya washindwe kushiriki kikamilifu katika siasa na kuwa na uwakilishi mzuri katika nafasi mbalimbali za uongozi na ufanyaji maamuzi.

Kwa upande mwingine, hatua chanya za kukuza haki ya kushiriki katika utawala ilichukuliwa na Serikali, baada ya Rais kuunda kikosi kazi cha kukusanya maoni kuhusu

demokrasia ya vyama vingi, ambacho kilitoa mapendekezo mbalimbali ya kuboresha demokrasia nchini, ikiwemo sheria kuruhusu matokeo ya uchaguzi wa urais kupingwa mahakamani, mara Mahakama ya Juu itakapoundwa; Sheria ya Vyama vya Siasa kurekebishwa ili kuvitaka vyama vya siasa kutengeneza sera za jinsia na ujumuishi; na katiba za vyama vya siasa kuingiza vifungu kuhusu usawa wa kijinsia na ukatili wa kijinsia.

Mwaka 2022 pia ulishuhudia haki ya wafungwa na mahabusu kupiga kura ikitetewa na kulindwa na mahakama, ambapo Mahakama Kuu ya Tanzania ilitoa hukumu kwamba kifungu cha 11(1)(c) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi kinakiuka haki ya wafungwa  na mahabusu ya kupiga kura na kutamka kwamba kifungu hicho kinaenda kinyume na Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977.

## 2.7. Uhuru dhidi ya Utesaji na Kutendwa kama siyo Binadamu

Kwa mwaka 2022, LHRC ilikusanya matukio takriban 44 ya utesaji na kutendewa kama siyo binadamu, ambayo ni matatu pungufu ya yale yaliripotiwa mwaka 2021. Matukio hayo yanajumuisha utesaji wa watuhmiwa walio chini ya ulinzi wa maafisa wa vyombo vya dola na utesaji wa watoto, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam, Shinyanga, Geita, Mara, na Iringa.

## 2.8. Uhuru dhidi ya Ukatili

Wanawake, watoto, wanaume, na watu wenye ulemavu walifanyiwa aina mbalimbali za ukatili mwaka 2022, ambazo zinakiuka haki yao ya uhuru dhidi ya ukatili. Wahanga wengi wa matukio ya ukatili walikuwa ni watoto na wanawake, hasa ukatili wa kingono na ukatili wa kimwili. Zaidi kidogo ya nusu ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake (asilimia  56) yaliyokusanywa na LHRC kupita utafiti wa taarifa za vyombo vya habari na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu yalikuwa ni ya ukatili wa kimwili na wa kihisia, wakati kwa upande wa watoto, asilimia 81 ya matukio ya ukatIli dhidi yao yalikuwa ni ukatili wa kingono. LHRC pia iliKusanya matukio 9 ya ukatili dhdi ya wanaume, ambayo ni ongezeko la matukio 2 ukilinganisha na matukio yaliyokusanywa mwaka 2021. Hali kadhalika, LHRC ilikusanya matukio 12 ya ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu na 24 ya ukatili dhidi ya wazee.

## 2.9. Haki ya Faragha

Mnamo mwezi Novemba 2022, Tanzania ilifuata nyayo za nchi jirani kama vile Kenya, Uganda,  na Rwanda kwa kutunga sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi.  Sheria ya  Ulinzi wa Taarifa Binafsi ilitungwa ili kuimarisha ulinzi wa taarifa  binafsi  za mtu na kumpatia nafuu

pale ambapo zimepatikana na/au kutumika kinyume na sheria, hivyo kulinda haki ya faragha na haki ya kuwa salama. Kabla sheria hii haijatungwa, wadau, zikwemo asasi za kiraia, waliuchambua muswada wa sheria hiyo na kutoa maoni kwa Bunge. Hata hivyo, ni asilimia 4 pekee ya mapendekezo 57 yaliyotolewa yalichukuliwa.

Pamoja na nia nzuri ya utungwaji wa sheria hiyo, wadau wamebaini mianya mbalimbali katika sheria hiyo, ikiwemo: maneno na vikundi vya maneno ambavyo havijaelezewa au kutafsiriwa vizuri, hivyo kuweza kutumika vibaya na mamlaka; matumizi ya lugha pana na maneno yasiyoeleweka vizuri; uhuru wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi; mamlaka ya Mwenyekiti na Tume kwa ujumla wake; wajiibu na uwajibikaji wa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi; mianya ya kijinsia; matakwa ya usajili; haki za kusikilizwa na kukata rufaa; na adhabu kali kwa kukiuka vifungu vya sheria.



03

SURA YA TATU:

# HAKI ZA KIUCHUMI, KIJAMII, NA KIUTAMADUNI

SURA YA TATU:

# HAKI ZA KIUCHUMI, KIJAMII, NA KIUTAMADUNI

## Utangulizi

Kwa mwaka 2022, hali ya haki za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni iliimarika kiasi ukilinganisha na mwaka 2021. Hii ilichangiwa na sababu mbalimbali, ikiwemo utengaji wa bajeti iliyoongezeka kidogo kwenye sekta muhimu kama vile elimu na afya, ajira kwa wafanyakazi wapya katika sekta hizo, na uongezaji wa viwango vya chini vya mshahara. Hata hivyo, utekelezaji na ufurahiaji madhubuti wa haki hizo uliendelea kuathiriwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo ufinyu wa bajeti; ucheleweshaji katika utoaji wa fedha za bajeti; fedha za bajeti kutotolewa zote; mazingira duni ya kazi; ukosefu wa ajira; upungufu wafanyakazi; upungufu wa vifaa, nyenzo, na majengo, ikiwemo madarasa; ubaguzi katika ajira; na aina tofauti za ukatili, hasa dhidi ya watoto, wanawake, na watu wenye ulemavu.

## 3.1. Haki ya Elimu

Serikali iliendelea kuchukua hatua mbailmbali kuhakikisha utekelezaji endelevu wa haki ya elimu, ikiwemo utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo na ujenzi wa madarasa mapya. Hata hivyo, bado kuna changamoto kadhaa katika elimu, ikiwemo ubora wa elimu; umbali wa shule; ufinyu wa bajeti; upungufu wa madarasa, walimu, vyoo, na vifaa na nyenzo nyingine za kujifunzia; ukatili dhidi ya watoto wanaosoma; ajira kwa watoto; mimba za utotoni; ndoa za utotoni; na wazazi kutotimiza wajibu wao na mahitaji ya watoto katika elimu.

### *Mazingira duni ya kufundishia na kujifunza*

Miongoni mwa vikwazo vya upatikanaji wa elimu bora nchini Tanzania ni pamoja na changamoto kama vile mazingira ya walimu ya kazi, ufinyu wa bajeti, upungufu wa walimu, upungufu wa madarasa, umbali

wa shule, mitaala iliyopitwa na wakati, changamoto ya hedhi salama miongoni mwa wasichana, na njaa na utapia mlo.

> *'Aisee watoto wanatembea umbali mrefu sana, hata mtu mzima huwezi, hivyo inapelekea watoto kuachishwa shule wakiwa tangu darasa la kwanza kwani hawawezi kutembea umbali mrefu.'*
>
> **Afisa ustawi, Katavi**

### *Changamoto zinazochangia watoto kutokuwa na umakini katika masomo*

Kuna changamoto kadhaa ambazo huwafanya watoto washindwe kutulia na kuijfunza. Mojawapo ya changamoto hizi kwa watoto wanaosoma shule nchini Tanzania ni njaa, kwani ni vigumu kwa mtoto kuwa makini darasani na kumsikiliza mwailmu kwa utulivu kama ana njaa. Kwa upande wa wavulana, uchezaji wa michezo ya video ulitajwa kama changamoto inaoyoathiri umakini wao na uzingatiaji wa masomo, hasa kwa watoto wanaoishi na kusoma katika maeneo ya mijini. Kwa wasichana, changamoto ya hedhi salama pia ilionekana kuathiri umakini na utulivu wao katika masomo, kwani bado shule nyingi hazina miundombinu rafiki kuwezesha hedhi salama.

### *Lugha ya kufundishia na mianya katika sera ya elimu*


Changamoto nyingine zilizoibuliwa kwa upande wa elimu kwa mwaka 2022 ni lugha ya kufundishia na mianya katika sera ya elimu. Wadau mbalimbali wa elimu waliendelea kuelezea wasiwasi wao kuhusu lugha ya kufundishia, kukiwa na mjadala mkali kuhusu matumizi ya Kiswahili au Kiingereza kama lugha ya kufundishia. Shirika la Haki Elimu pia lilifanya uchambuzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, ambao ulifanyika mwaka 2021, na kubainisha mianya mbalimbali katika sera hiyo na kutoa mapendekezo ya kuboresha sera. Hata hivyo, mwaka 2022, Serikali ilitangaza kuanza kufanya mapitio ya sera hiyo.

**Wito wa LHRC:** Serikali izingatie mapendekezo yaliyotolewa na Shirika la Haki Elimu katika uchambuzi wake wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014.

### *Utengaji wa bajeti*

Bado bajeti inayotengwa kwa ajili ya sekta ya elimu haitoshelezi na haikidhi kiwango cha kimataifa kuhusu bajeti ya elimu, ambacho ni asilimia 20 ya bajeti ya nchi kutengwa kwa ajili ya elimu. Kwa mwaka wa fedha 2022//23, kiasi cha bajeti kilichotengwa kwa ajili ya sekta ya elimu kilikuwa ni asilimia

13.7 ya bajeti yote. Changamoto nyingine zinazohusiana na bajeti ni ucheleweshaji katika utoaji wa fedha za bajeti na kiasi cha fedha za bajeti kutotolewa, hali ambayo inaathiri utoaji wa huduma ya elimu bora.




*Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya sekta ya elimu kwa miaka ya fedha fedha 2018/19 hadi 2022/23 na asilimia yake katika bajeti ya taifa*

## Ukatili dhidi ya watoto wanaosoma shule

Mwaka 2022 baadhi ya watoto wanaosoma shule walifanyiwa vitendo mbalimbali vya ukatili wa kingono,kimwili, kisaikolojia, na kiuchumi, na kuwafanya washindwe kufurahia na kutekeleza vizuri haki yao ya elimu. Adhabu ya viboko iliendelea pia kutumika katika shule mbalimbali, huku wadau wakiendelea kutofautiana kuhusu matumizi ya adhabu hiyo. Baadhi ya wadau wamekuwa wakidai ifutwe kwa sababu ni ya kikatili, huku wengine wakiona ni bora indelee kuwepo. Utekelezaji adhabu ya viboko ulileta madhara mkoani Mtwara, baada ya mwanafunzi, Amina Ally (16), kudaiwa kufariki baada ya kuchapwa na mwalimu kwa kushindwa kutoa jibu sahihi la swali aliloulizwa.

## Ndoa na mimba za utotoni

Ndoa na mimba za utotoni ziliendelea kuwa mwiba kwa ndoto za wasichana wengi kwa upande wa elimu. Ndoa za utotoni, ambazo bado zinaruhusiwa katika Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, ziliendelea kuwa tishio kwa haki za wasichana, ikiwemo haki ya kupata elimu, kwa sababu bado Serikali haijachukua hatua kufanya marekebisho ya sheria hiyo ili kulinda haki na ustawi wa msichana.

## Wazazi kuwashawishi watoto wao kufeli mitihani

Katika baadhi ya maeneo katika mikoa nchini, LHRC imebaini kwamba kuna wazazi ambao wamekuwa wakiwashawishi watoto wao kufanya vibaya katika mitihani yao ili wafeli na wasiendeee na masomo. Kwa mwaka 2022, taarifa kuhusu tabia hii ya baadhi ya wazazi iliriopotiwa katika Mikoa ya Songwe, Geita, Njombe, Katavi, na Shinyanga. Sababu kuu ya kutaka mtoto wa kike kufeli ni ili aolewe.

*'Yaani watoto wengi wenye uwezo mkubwa sana darasani ambao tulikuwa tunawategemeea sana darasani natukaona performance yao inashuka kila siku tukaitisha kikao kikao cha wazazi pamoja na mtendaji wa kijiji na kata ndio ikagundulika wazazi wanawatishia watoto wao kwamba watakapofaulu wao wazazi watakufa.'*

**Mwalimu - Njombe**

*'Watoto wanalazimishwa na wazazi wao kufanya vibaya kwenye mitihani yao ili waozeshwe au kufanya kazi ili kulisha familia nzima.'*

**Mfanyakazi asasi ya kiraia – Nsimbo, Katavi**

## 3.2. Haki ya Afya

Kwa mwaka 2022, Serikali iliendelea kuchukua hatu mbalimbali kuhakikisha utekelezaji wa haki ya afya kulingana na rasilimali zilizopo, na kutatua baadhi ya changamoto katika sekta ya afya, ikiwemo kuajiri wafanyakazi wapya, ujenzi wa vituo vya afya na hospitali, na manunuzi na usambazaji wa madawa na vifaa tiba muhimu. Hata hivyo, changamoto mbalimbali ambazo ziliathiri utekelezaji madhubuti wa haki ya afya ziliripotiwa, ikiwemo ufinyu wa bajeti; upungufu wa wafanyakazi; afya ya akili na watu kujiua; ukatili dhidi ya wanawake na wasichana; upungufu wa mashine, madawa, na vitaa tiba; na changamoto zinazohusiana na afya ya uzazi.

### *Bajeti ya sekta ya afya*

Kupitia Tamko la Abuja, nchi mbalimbali za barani Afrika, ikiwemo Tanzania, zilijiwekea dhamira ya kutenga asilimia 15 ya bajeti ya nchi kwa ajili ya sekta ya afya. Hata hivyo, kwa wastani, asilimia ya bajeti ya sekta hiyo katika bajeti ya taifa imekuwa ni asilimia 5.84 pekee katika vipindi vya miaka ya fedha mitano iliyopita (2018/19 to 2022/23).




*%Bajeti iliyotengwa na Serikali kwa ajili ya sekta ya afya ukilinganisha na lengo kwa miaka ya fedha 2018/19 hadi 2022/23*

**Mtazamo & Wito wa LHRC:** Ili kukidhi viwango vya kimataifa na kuyafikia malengo mbalimbail kuhusu afya, Serikali haina budi kuchukua hatua ya kuongeza zaidi bajeti kwa ajili ya sekta ya afya. Pia, Serikali ihakikishe kwamba fedha za bajeti zinatolewa kwa wakati kwa wizara na taasisi husika ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora za afya.

### *Upungufu wa wanyakazi, vifaa, na madawa*

- Pamoja na juhudi mbalimbali za Serikali za kuajiri wafanyakazi wapya katika sekta ya afya, bado sekta hiyo inakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi. Mathalani, mwaka 2022 iliripotiwa kwamba Hospitail ya Taifa ya Muhimbili ilikuwa ikikabiliwa na upungufu wa takribani asilimia 40 ya wafanyakazi, huku madaktari wa meno pia wakiripotiwa kuwa pungufu katika maeneo mbailmbali nchini.
- Upungufu wa vifaa, madawa, na vifaa tiba pia uliendelea kuwa changamoto katika utekelezaji madhubuti wa haki ya afya kwa mwaka 2022.

### *Wasiwasi kuhusu bima ya afya*

Kutokuwa na bima ya afya ni changamoto kubwa kwa Watanzania wengi. Hata hivyo, mwaka 2022 ulileta matumaini kidogo katika hili baada ya Serikali kuleta muswada wa bima ya afya kwa wote, lakini jitihada kubwa zinahitajika ili kuweza kuleta sheria nzuri ya bima ya afya kwa wote.


**Wito wa LHRC:** Bunge la Tanzania kuwashirikisha kikamilifu wadau wote wa afya na haki ya afya, zikiwemo asasi za kiraia, katika mchakato wa kutunga sheria na kuleta mfumo wa bima ya afya kwa wote, kwa kuzingatia maoni na mapendekezo ya wadau na kutumia mtazamo wa haki za binadamu. Pia, Serikali iharakishe mchakato huo na kuleta bima ya afya kwa wote ili kuimarisha haki ya afya.

### *Afya ya akili na matukio ya watu kujiua*

Afya ya akili ni mojawapo ya masuala ambayo yalijadiliwa sana Tanzania Bara kwa mwaka 2022, ambapo wadau mbalimbali,wakiwemo madaktari, walielezea wasiwasi wao kuhusu hali ya afya akili miongoni mwa raia. Mnamo mwezi Julai mwaka 2022, Dkt. Omary Obuguyu, ambaye ni daktari kutoka Wizara ya Afya, alisema kwamba kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wa afya ya akili katika miaka mitano iliyopita.

Jijini Mwanza, wanasaikolojia na wataalamu wa maendeleo ya jamii walisema kwamba afya ya akili ni kisababishi kikuu cha matukio ya watu kujiua nchini Tanzania. Kwa mwaka 2022, LHRC ilikusanya matukio matatu ya watu kujiua kupitia utafiti wa taarifa za vyombo vya habari na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu, ambayo yamepungua kutoka matukio 45 mwaka 2021. Uchambuzi wa matukio hayo ulionyesha kwamba wahanga wengi (asilimia 83) ni wanaume, wakiongezeka kutoka asilimia 76 mwaka 2021. Ni asilimia 17 pekee ya wahanga ndiyo walikuwa ni wa kike, nusu yao wakiwa ni wasichana. Kwa upande wa umri, wahanga

wengi walikuwa ni vijaa (miaka 18 hadi 35), ambao walikuwa ni asilimia 40 ya wahanga.




*Asilimia ya matukio ya watu kujiua kwa umri*

Sababu zilizotajwa za watu kujiua ni pamoja na: migogoro ya kifamilia, mshahara kuzuiliwa kama adhabu, madeni, wivu, kugombezwa na mzazi, maumivu ya kuachwa na mpenzi, kutuhumiwa kufanya uhalifu, kupoteza vitu, na kupoteza fedha.

### *Afya ya uzazi*

Utekelezaji wa haki za afya uzazi, hasa kwa upande wa vijana, uliendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo upatikanaji wa huduma bora za afya kwa akinamama wajawazito na ukatili dhidi ya wanawake na wasichana. Mathalani, baadhi ya wanawake na wasichana walifanyiwa vitendo mbalimbali vya ukatili, ikiwemo ubakaji, ulawiti (ikiwemo ulawiti ndani ya ndoa), na ukeketaji, ambao ulihatarisha haki zao za afya ya uzazi.

## 3.3. Haki ya Maji Safi na Salama

Pamoja na juhudi mbalimbali za kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa haki ya maji, bado kuna changamoto kubwa za upatikanaji wa maji safi na salama katika baadhi ya maeneo nchini, ikiwemo, ufinyu wa bajeti iliyotengwa kwa ajili ya sekta ya maji; uvujaji na upotevu wa maji; maji kutopatikana kirahisi katika baadhi ya maeneo, hasa vijijini; mgao wa maji; na athari za mabadiko ya tabianchi.


## 3.4. Haki ya Kufanya Kazi

Masuala makuu yalioathiri haki ya kufanya kazi mwaka 2022 kwa upande wa Tanzania Bara ni pamoja na kuletwa kwa Waraka Mpya wa Viwango vya Chini vya Mishahara; upungufu wa wafanyakazi katika sekta muhimu; na ukiukwaji wa haki za wafanyakazi, hasa katika sekta ya biashara.

### *Waraka mpya wa Viwango vya Chini vya Mshahara*

Uletwaji wa Waraka mpya wa Viwango vya Chini vya Mshahara mwaka 2022 ulikuwa ni habari njema kwa upande wa haki za wafanyakazi, kwani waraka huu umesubiriwa muda mrefu, tangu mwaka 2013. Wanufaika wakuu wa ongezeko la viwango vya

mshahara ni wafanyakazi wa majumbani waliojiriwa na mabalozi na wafanyabiashara wakubwa, ambao kiwango chao cha chini cha mshahara kiliongezeka kwa asilimia 67, wakifuatiwa na wafanyakazi wa majumbani walioajiriwa na maafisa wakubwa (asilimia 54), na wafanyakazi katika vyombo vya habari, posta, na huduma za usafirishaji wa vifurushi (asilimia 50).




*Asilimia kubwa za ongezeko la viwango vya chini vya mishahara (asilimia 48 hadi 67) katika Waraka wa Viwango vya Chini vya Mshahara wa mwaka 2022*

Ongezeko dogo zaidi katika viwango vya chini vya mshahara lilikuwa ni mshahara wa wafanyakazi wa migahawa, nyumba za kulala wageni, na baa (asilimia 15), wafanyakazi katika uvuvi na huduma za majini (asilimia 19), wafanyakazi katika hoteli kubwa na za kitalii (asilimia 20), wafanyakazi katika hoteli za kati (asilimia 20), wafanyakazi katika huduma ya ugomboaji na uondoshaji mizigo (asilimia 20), wafanyakazi katika huduma za mawasiliano (asilimia 25), leseni za uchimbaji wa kati na za utafutaji wa madini (asilimia 25), leseni Ndogo (asilimia 25), ujenzi (asilmia 28 hadi 29), na usafiri wa angani (asilimia 30).

**Wito wa LHRC:** Serikali, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Watu wenye Ulemavu), kuhakiisha utekelezaji madhubuti wa Waraka mpya wa Viwango vya Chini vya Mishahara katika sekta ya biashara. Pia, Serikali ihakikishe waraka huo unafanyiwa mapitio kwa wakati muda utakapofika (kila baada ya miaka 3), ili tuweze kupata waraka mpya mwaka 2025.

### *Ukiukwaji wa haki za wafanyakazi*

Ukiukwaji wa haki za wafanyakazi uliendelea kuwa changamoto mwaka 2022, hasa katika sekta ya biashara. Vitendo vya ukiukwaji wa haki hizo vilikuwa ni pamoja na kutolipwa kwa kufanya kazi muda wa ziada; kufanyishwa kazi kupita kiasi na kutolipwa ipasavyo; ubaguzi; ucheleweshaji wa malipo ya mishahara; ukatili mahala pa kazi; kutowasilishwa kwa michango ya hifadhi ya jamii; kukataliwa kwenda likizo; kufukuzwa kazi kinyume na utaratibu; na kutopata mafunzo ya afya na usalama kazini.

Wafanyakazi katika sekta kama elimu na afya katika taasisi mbalimbali za umma pia walikabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo mazingira duni ya kazi, hasa katika maeneo ya vijijini.

LHRC ilikusanya matukio takribani 50 ya ukiukwaji wa haki za wafanyakazi katika kipindi cha Januari hadi Juni 2022 pekee,kupitia programu zake za ufuatiliaji wa haki za binadamu na msaada wa kisheria. Kesi nyingi zilikuwa ni za usitishaji wa ajira kinyume na utaratibu, kutolipwa mshahara, na kutopelekwa kwa michango ya wafanyakazi katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

**Mtazamo wa LHRC:** Kwa sababu mojawapo ya sifa za haki za binadamu ni kutegemeana, ukiukwaji wa haki za wafanyakazi siyo tu unakiuka haki ya kufanya kazi, bali pia unaweza kusababisha ukiukwaji wa haki nyingine kama vile haki ya kuishi katika hali inayofaa, haki ya afya, haki ya elimu, haki ya usawa mbele ya sheria, na haki ya kuwa huru na salama.

**Wito wa LHRC:** Serikali, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Watu wenye Ulemavu), kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa sheria na kanuni za kazi kulinda haki za wafanyakazi.


### 3.5. Haki ya Kumiliki Mali

Kwa mwaka 2022, masuala makuu yaliyoathiri utekelezaji wa haki ya kumiliki mali ni pamoja na: migogoro ya ardhi; ukiukwaji wa haki za wanawake kutumia na kumiliki mali; unyang'anyi wa mali kutoka kwa wajane na wazee; na utatuzi wa migogoro.

Washiriki wa utafiti wa haki za binadamu waliulizwa kuhusu namna wanavyoridhishwa na ulinzi wa haki ya kumiliki mali, ambapo wengi wao (asilimia 48) walisema kwamba wanaridhishwa kiasi, wakifuatiwa na robo ambao walisema wanaridhishwa, na asilimia 18 ambao walidai kwamba hawaridhishwi. Zaidi kidogo ya nusu ya washiriki (asilimia 52) pia walitaja migogoro ya mipaka kama aina kuu ya migogoro ya ardhi katika jamii yao, wakifuatiwa na asilimia 18 ambao walitaja migogoro kati ya wakulima na wafugaji, huku asilimia 16 wakitaja migogoro kati ya wanajamii na wawekezaji.

Mwaka 2022 LHRC ilugundua pia masuala kadhaa kuhusu ardhi wakati wa utoaji wa msaada wa kisheria kwa wateja kutoka katika sehemu mbalimbali za Tanzania Bara. Masuala hayo ni pamoja na uelewa mdogo kuhusu masuala na sheria za ardhi miongoni mwa wanajamii; uelewa mdogo kuhusu marekebisho mbalimbali yaliyofanywa katika Sheria ya Sheria ya Migogoro ya

Ardhi, Sura Namba 216 miongoni mwa wajumbe wa mabaraza ya kati; na uingiliaji wa kisiasa katika mashauri ya migogoro ya ardhi. Data za msaada wa kisheria za LHRC pia zinaonyesha kwamba kwa mwaka 2022 migogoro ya ardhi iliongoza katika migogoro iliyopokelewa (asilimia 41), ikifuatiwa na ajira (asilimia 22), na migogoro ya kifamilia (asilimia 18).




*Kesi za msaada wa kisheria zilizopokelewa na LHRC mwaka 2022 kwa aina ya mgogoro*

Kwa mwaka 2022, LHRC ikusanya tribani matukio tisa ya migogoro ya ardhi, kupitia programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu na utafiti wa taarifa za vyombo vya Habari. Matukio haya yaliripotiwa katika Mikoa ya Arusha, Lindi, Kilimanjaro, Kigoma, Singida, na Morogoro. LHRC pia ilikusanya matukio 13 ya unyang'anyi wa mali za wanawake na wazee,ambayo yaliripotiwa katika mikoa kama vile Kilimanjaro, Njombe, Tanga, na Kigoma.

Katika jamii nyingi za vijijini, bado wanawake wananyimwa haki ya kumiliki ardhi, huku wanaume wakiwa na maamuzi ya mwisho katika upatikanaji na matumizi ya ardhi. Hali hii inaathiri uwezo wa wanawake kujikwamua kiuchumi, ikiwemo kuweza kupata mitaji na mikopo, na inachangiwa zaidi na mila na desturi zinazowabagua wanawake. Mila hizi zimekumbatiwa zaidi na wanaume na watu waliotoka katika kaya maskini na walio na elimu ndogo.

> *'Suala la mwanamke kumiliki mali au ardhi lipo nyuma sana..pindi mume akifariki ndugu humfukuza mwanamke arobaini ikiisha tu, na tatizo linakuja hakuna mabaraza ya kata na kijiji angalau yangesolve matatizo ya ardhi.'*
> **Mfanyakazi asasi ya kiraia – Nsimbo, Katavi**

## 3.6. Haki ya Kuishi katika Hali Inayofaa

Kwa mwaka 2022, masuala makuu yaliyoathiri haki ya kuishi katika hali inayofaa kwa upande wa Tanzania Bara ni pamoja na upungufu wa chakula, unaochangiwa na athari ya mabadiliko ya tabianchi; upatikanani wa chakula chenye virutubisho; uwezo wa kumudu gharama za chakula; upatikanaji wa makazi yanayofaa; na ulinzi wa haki za mpangaji katika nyumba au ardhi.

### *Upungufu wa chakula*

Upungufu wa chakula ulisemekana kuwa

changamoto katika baadhi ya maeneo ya Tanzania Bara, ukisababishwa zaidi na kutokuwepo kwa mvua za kutosha, hivyo kupunguza kasi ya uzalishaji wa chakula na mifugo kwa sababu ya kutokuwepo kwa maji na malisho ya kutosha. Hali hii ilisibabishwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya tabianchi, ambayo yamekuwa yakiathiri kilimo, uwepo wa chakula, na lishe nchini Tanzania


### *Upatikanaji wa chakula chenye virutubisho*

Kaya nyingi nchini Tanzania zimekuwa zikipata wakati mgumu kuweza kumudu kupata vyakula vyenye virutubisho. Hata hivyo, kwa mwaka 2022, Tanzania ilionekana kuendelea kupiga hatua katika kutatua changamoto hii, kwa mujibu wa Ripoti ya Dunia ya Virutubisho. Pia, kwa mujibu wa Utafiti wa Kidemografia na Afya na Utafiti wa Viashiria vya Malaria wa mwaka 2022, asilimia ya watoto wenye umri chini ya miaka 5 wenye udumavu imepungua kutoka asilimia 48 mwaka 1999 hadi asilimia 30 mwaka 2022.


Kwa mwaka 2022, gharama za chakula, ambazo ziliongezeka, pia zilikuwa tishio kwa haki ya chakula, sambamba na changamoto za migao ya maji na umeme.

### *Bajeti kwa ajili ya sekta ya kilimo*

Mwaka 2022 wadau mbalimbali wa kilimo walielezea wasiwasi wao kuhusu bajeti isiyotosheleza inayotengwa kwa ajili ya sekta kilimo, ambayo imekuwa haifikii kiwango cha asilimia 10 ya bajeti nzima kilichopendekezwa katika Tamko la Malabo la Umoja wa Afrika la mwaka 2014. Pia,wadau walilalamika kuhusu ucheleweshaji wa fedha za bajeti. Hata hivyo, kwa mwaka fedha 2022/23, kulikuwa na matumaini kwa upande wa bajeti kilimo, baada ya serikali kuongeza bajeti hiyo kwa kiasi kikubwa, ikiwemo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.




*Asilimia ya bajeti ya kilimo kwenye bajeti ya taifa katika miaka ya fedha 2016/17 hadi 2022/23*
*Chanzo:Wizara ya Fedha na Mipango & Shirika la Policy Forum*




*Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya sekta ya kilimo – 2021/22 & 2022/23*
*Chanzo:Wizara ya Fedha na Mipango & Shirika la Policy Forum*

*Upatikanaji wa nyumba bora*

Upatikanaji wa nyumba bora za kuishi bado ni changamoto kwa Watanzania katika maeneo mbalimbali ya mijini na vijijini. Wanawake na watu wengine walio katika makundi maalum wanaathirika zaidi na ukosefu wa nyumba bora. Pia, ukosefu wa nyumba bora kwa upande wa wanawake unachangiwa na sababu mbalimbali, ikiwemo kunyimwa haki za urithi sababu ya baadhi ya mila zinazowabagua; unyang'anyi wa mali; na kutoweza kutumia na/au kumiliki ardhi. Sheria za kimila zimeendelea kuwa tishio kwa haki za wanawake na wasichana za kumiliki mali na kurithi, hivyo kuathiri pia haki ya kuishi katika nyumba bora.

**Mtazamo wa LHRC:** Makazi na nyumba bora vina umuhimu mkubwa katika ufurahiaji na utekelezaji wa haki nyingine za binadamu. Hata hivyo, bado watu wengi wanakabiliwa na changamoto ya kuishi katika nyumba zisizo bora, kote mijini na vijijini. Wahanga wakuu katika hili ni wanawake, watoto, na makundi mengine maalum.

**Wito wa LHRC:** Serikali, kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi, kuongeza juhudi za kuboresha makazi na kuhakikisha upatakanaji wa nyumba bora za kuishi. Juhudi za pamoja na za kisekta zinahitajika katika kushughulikia changamoto hii. Pia, Serikali haina budi kurekebisha sheria za kimila zinazobagua wanawake ili kulinda haki zao za kumiliki mali, urithi, na nyumba bora.

## 3.7. Haki ya Ulinzi wa Kijamii

Pamoja na Serikali kuchukua hatua mbalimbali kulinda haki ya ulinzi wa kijamii, ikiwemo uanzishaji wa mifuko ya hifadhi ya jamii, utoaji wa mikopo kwa vikundi, na utekelezaji wa programu ya ulinzi wa kijamii ya TASAF, bado Watanzania wengi hawajalindwa na ulinzi wa kijamii, hasa wale waliokuwa katika sekta isiyo rasmi. Changamoto nyingine zinazohusiana na haki hii ni pamoja na upatikanaji wa pensheni kwa wazee, kufa kwa ulinzi wa kijamii wa kitamaduni, vipato vidogo vya watu, upatikanaji wa huduma bora za afya na vyakula vyenye virutubisho kwa wazee, vijana kutowajibika kuwatunza wazee, changamoto za mafao ya uzazi na ulinzi wa kazi katika sekta ya biashara, na upelekaji wa michango ya wafanyakazi katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

**Wito wa LHRC:** Serikali, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Watu wenye Ulemavu), kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa sheria za ulinzi wa kijamii na kuhakikisha waajiri wanapeleka michango ya kila mwezi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.



04

SURA YA NNE:

# HAKI ZA KIUJUMLA

SURA YA NNE:

# HAKI ZA KIUJUMLA

## Utangulizi

Kwa mwaka 2022, masuala makuu yaliyoathiri haki mbalimbali za binadamu, kama zilivyoelezewa katika sura zilizotangulia, pia yaliathiri haki za kiujumla, ikiwemo haki ya maendeleo.

## 4.1. Haki ya Maendeleo

Kwa mwaka 2022, masuala makuu yaliyoathiri haki ya maendeleo ni pamoja na ukiukwaji wa haki za binadamu, hasa haki za kiraia na kisiasa, na changamoto katika utoaji wa huduma za kijamii na kimahakama, ikiwemo za ufinyu wa bajeti na upungufu wa rasilimali watu.Rushwa, ambayo ni kikwazo kikubwa zaidi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, pia iliendelea kuwa tishio katika utekelezaji wa haki ya maendeleo.

## 4.2. Haki ya Kufurahia na Kufaidika na Maliasili

Pamoja na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Serikali kuhakikisha ufurahiaji wa haki ya kufurahia na kufaidika na maliasili, bado kuna changamoto kadhaa ambazo zinazuia utekelezaji madhubuti wa haki hii, ikiwemo rushwa, misamaha ya kodi, na ukwepaji kodi, hasa katika sekta ya uziduaji. Hali imesababisha wanajamii wengi katika maeneo yenye maliasili, kama vile madini, kubaki katika lindi la umaskini.

## 4.3. Haki ya Mazingira Safi na Salama

Wanajamii walioshiriki katika utafiti wa haki za binadamu na biashara, uliofanywa na LHRC katika mikoa 14 ya Tanzania Bara mwaka 2022, walitaja uchafuzi wa hewa kama changamoto kubwa zaidi ya uchafuzi wa mazingira (asilimia 40.5), ukifuatiwa na uchafuzi wa ardhi (asilimia 27), uchafuzi wa maji (asilimia 21.7), na kelele (asilimia 10.8). Kupitia utafiti huu, LHRC ilikusanya matukio 37 ya uchafuzi wa mazingira, ikiwemo uchafuzi wa Mto Mara mkoani Mara, ambao ulileta mjadala mkubwa kitaifa. Mkoani

Tanga, yaliyotolewa malalamiko kuhusu uchafuzi wa hewa kupitia vumbi dhidi ya Kampuni ya Neelkanth Lime Ltd., iliyopo katika Kata ya Kiomoni katika Manispaa ya Tanga. Mkoani Dar es Salaam, kulikuwa na malalamiko kuhusu uchafuzi wa mazingira unaofanywa na viwanda, hususan uchafuzi wa hewa, katika maeneno ya viwanda ya Mikocheni. Mkoani Mbeya, malalamiko mengi yalikuwa ni kuhusu uchafuzi wa hewa unaosababishwa na shughuli za viwanda vya kukoboa mpunga, hasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.

Kupitia utafiti wa taarifa za vyombo vya habari, LHRC pia ilikusanya matukio ya kelele, ambayo yaliripotiwa katika mikoa kama vile Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Morogoro, Tanga, Mbeya, Iringa, Mwanza, na Mara. Kufuatia hali hii, wadau mbalimbali waliliomba Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuingilia kati na kutokomeza aina hii ya uchafuzi wa mazingira, ambayo imekuwa ikisababisha kero kwa wananchi, ikiwemo katika maeneo yenye baa na kumbi za starehe.



05

SURA YA TANO:

# HAKI ZA MAKUNDI MAALUM

SURA YA TANO:

# HAKI ZA MAKUNDI MAALUM

## Utangulizi

Kwa mwaka 2022, makundi maalum, ikiwemo wanawake, watoto, na watu wenye ulemavu, waliendelea kufurahia haki zao mbalimbali kama binadamu, kama zilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mikataba mbalimbali ya kimataifa ya haki za binadamu. Hata hivyo, baadhi yao walifanyiwa vitendo mbalimbali vya ukiukwaji wa haki za binadamu, ikiwemo ukatili wa kijinsia na ubaguzi.

## 5.1. Haki za Wanawake


Ukiacha mikataba mbalimbali ya haki za binadamu inayotoa ulinzi wa haki za binadamu kwa watu wote, kuna mikataba kadhaa ambayo ni maalum kwa ajili ya kulinda haki za wanawake. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Wanawake (Maputo Protocol) wa mwaka 2003. Jambo kubwa linalokatazwa katika mikataba hii ni ubaguzi dhidi ya wanawake - unaopelekea kushindwa kufurahia haki zao muhimu kama binadamu. Pia, mikataba hii inakataza aina zote za ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake.

### *Mienendo na matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake*

Kwa mwaka 2022, ukatili wa kijinsia uliendelea kuwa tishio kwa haki za wanawake nchini Tanzania. Matukio ya aina mbalimbali za ukatili, ikiwemo ukatili wa kimwili, kisaikolojia, na kiuchumi, yaliripotiwa katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.


Takwimu za polisi za ukatili wa kijinsia zinaonyesha kwamba matukio yaliyoripotiwa yalipungua kutoka 42,414 mwaka 2020 hadi 29,373 mwaka 2021, sawa na upungufu wa asilimia 30.8. Hata hivyo, kwa mwaka 2022 polisi katika mikoa mbalimbali waliripoti

kwamba matukio ya ukatili wa kijinsia yaliongezeka. Mathalani, mnamo mwezi Oktoba mwaka 2022, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Katavi, Ali Makame, alisema kwamba matukio ya ukatili wa kijinsia yaliyoriptiwa katika kipindi cha Janauri hadi Septemba yaliyokuwa ni 270, yakiongezeka kutoka matukio 240 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021.




*Wahanga wa ukatili wa kijinsia nchini Tanzania kwa jinsi – 2018 hadi 2021*
*Chanzo: Takwimu za polisi, 2018 hadi 2021*

Kupitia utatifii wa taariza za vyombo vya habari na progamu yake ya ufuatiliaji wa haki za binadamu, LHRC ilikusanya matukio takribani 108 ya ukatili dhidi ya wanawake, ambayo yalliripotiwa katika mikoa kama vile Pwani, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Mara, Mtwara, Rukwa, Songwe, Geita, Dodoma, na Kigoma. Asilimia 56 ya matukio hayo yalikuwa ni ya ukatili wa kimwili na kihisia, yakifuatiwa na ukatili wa kingono (asilimia 28), na ukatili wa kiuchumi (asilimia 16).




*Asilimia ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2022 kwa aina ya ukatili*

Matukio ya ukatili dhidi ya wanawake pia yaliripotiwa katika mikoa yote 20 iliyotembelewa na LHRC wakati wa ufanyaji wa utafiti wa haki za binadamu, ambapo jumla ya matukio 1,391 yalikusanywa. Asilimia 46 ya matukio yalikuwa ni ya ukatili wa kimwili na kisaikolojia, asilimia 29 yalikuwa ni ya ukatili wa kingono (ikiwemo ubakaji na rushwa ya ngono), na asilimia 25 iliyobakia ilikuwa ni matukio ya ukatili wa kiuchumi. Wanajamii wengi waliohojiwa, wakiwemo maafisa ustawi wa jamii, wasaidizi wa kisheria, na waangalizi wa haki za binadamu, pia walisema kwamba aina ya ukatili ambayo wanawake wanakumbana nayo zaidi ni ukatili wa kimwili, ukifuatiwa na ukatili wa kiuchumi.

> ***'Kwa kweli ukatili wa kimwili dhidi ya wanawake ni tatizo kubwa sana, hasa kwa wenza au wanandoa."***

**Msaidizi wa kisheria – Manispaa ya Moshi, Kilimanjaro**

**Mtazamo wa LHRC:** Ni wakati muafaka sasa kwa Tanzania kutunga sheria maalum ya kupinga ukatili wa kijinsia. Tunaweza kujifunza kutoka kwa nchi mbalimbali duniani ambazo tayari zimeshatunga sheria hii, ikiwemo Bulgaria, Afrika Kusini, Malaysia, India, Sierra Leone, na Namibia.

**Wito wa LHRC:** Serikali itunge sheria ya kupinga ukatili wa kijinsia ili kuongeza juhudi za mapambano dhidi ya ukatili huo kulingana na matakwa ya viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.


## *Mtazamo wa wanajamii kuhusu ukatili dhidi ya wanawake*

Zaidi ya nusu ya wanajamii walioshiriki kwenye utafiti wa haki za binadamu (asilimia 44), walisema kwamba ukatili dhidi ya wanawake ni tatizo kubwa katika jamii yao, wakifuatiwa na asilimia 29 waliosema kwamba ni tatizo, na robo waliodai ni tatizo kiasi.




*Mtazamo wa wanajamii kuhusu tatizo la ukatili dhidi ya wanawake*

Kimkoa, asilimia ya washiriki waliosema kwamba ukatili dhidi ya wanawake ni tatizo kubwa ilikuwa kubwa zaidi katika Mkoa wa Dodoma (asilimia 84) na ndogo zaidi katika Mkoa wa Katavi (asilimia 58). Kikanda, Kanda ya Kaskazini (Tanga, Kilimanjaro, na Arusha), ilikuwa na wastani wa juu zaidi (asilimia 82), ikifuatiwa na Kanda ya Kati (Morogoro, Dodoma, Tabora, na Singida), iliyopata asilimia 76, na Kanda za Mashariki (Dar es Salaam, Pwani & Mtwara) na Magharibi (Rukwa, Kigoma, na Katavi), ambazo zote zilipata asilimia 70.




*Mikoa 5 ambayo ukatili dhidi ya wanawake ulionekana kuwa tatizo kubwa*

## Ukatili dhidi ya wanawake na wasichana mtandaoni

Wanawake pia wanaweza kuwa wahanga wa ukatili mtandaoni, kama ilivyo kwa aina nyingine za ukatili. Hata hivyo, tafiti zinaonyesha kwamba wanawake na wasichana wapo katika hatari zaidi ya kufanyanyiwa aina hii ya ukatili, ambao husababisha madhara ya kimwili, kisaikolojia, au kiuchumi. Aina hii ya ukatili imekuwa ikichukuliwa kama siyo kubwa na isiyo na madhara sana kwa wahanga kwa sababu siyo mara zote inasababisha madhara ya kimwili, lakini ukweli ni kwamba ukatili mtandaoni una madhara makubwa pia, wakati mwingine ukipelekea ukatili wa kimwili na kuchangia changamoto za afya ya akili kama vile sonona na ugonjwa wa wasiwasi (hofu). Aina hii ya ukatili pia inasababisha wahanga kujiondoa katika majukwaa mbalimbali mitandaoni na wengine kujiondoa kabisa mitandaoni, suala ambalo lina athari kubwa katika kujiamini kwa wanawake kwenye masuala la TEHAMA, hivyo kuchangia kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia mtandaoni. Vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake mtandaoni ni pamoja na kumfuatilia na kumwangalia mtu mtandaoni kupita kiasi, unyanyasaji mtandaoni, uonevu mtandaoni, kauli za chuki, na matumizi ya picha ya mtu ya faragha mtandaoni bila ridhaa yake

Kwa mwaka 2022, wadau mbalimbali, akiwemo Mh. Neema Lugangira (Mbunge), walielezea wasiwasi wao kuhusu ukatili dhidi ya wanawake mtandaoni na kuomba aina hii ya ukatili iingizwe katika Mpango Kazi mpya wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto. Mh. Neema Lugangira alisema kwamba ukatili wa kijinsia unaofanywa katika mitandao unashika kasi na ni wakati sasa wa kufanya jitihada wa kukabiliana na tatizo hili. Alisema pia kwamba wahanga wakuu wa ukatili huu ni pamoja na wasichana, wajasiriamali, viongozi wa kisiasa wanawake, na wabunge wanawake.


**Mtazamo wa LHRC:** Katika dunia ya leo, upatikanaji wa wavuti na matumizi ya mitandao na majukwaa ya kijiditali imekuwa ni suala la lazima kwa maendeleo ya kiuchumi

na muhimu katika utekelezaji wa haki za binadamu. Hivyo basi, mtandao unatakiwa kuwa sehemu salama kwa kila mtu, ikiwemo wanawake na watoto; na ulinzi wa haki za msingi za binadamu, ikiwemo uhuru wa kujieleza, uhuru dhidi ya ukatili na haki ya kuwa huru na salama, unatakiwa kupanuliwa hadi kwenye majukwaa ya mtandaoni.

**Wito wa LHRC:** Kuna haja ya Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kufanya marekebisho ya kisheria na kisera kuhakikisha ukatili dhidi ya wanawake na watoto mtandaoni unaingizwa kikamilifu katika sheria na sera, sambamba na kutekeleza programu za uenezaji uelewa wa umma. Pia, kuna haja ya kufanya utafiti zaidi kwenye suala hili la ukatili dhidi ya wanawake na watoto mtandaoni.

### *Ukatili dhidi ya mwenza na mauaji ya mwenza: Ukatili wa kimwili dhidi ya wanawake unaokua*

Karibia nusu ya wanawake nchini Tanzania (asilimia 48) wamewahi kufanyiwa ukatili na wenza wao, na mwanamke mmoja kati ya wanne amefanyiwa ukatili na mwenza wake katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Katika miaka ya hivi karibuni, ukatili dhidi ya mwenza umesababisha matukio mengi ya mauaji ya mwenza yanayofanywa na mwenza. Kwa mwaka 2022, LHRC ilikusanya matukio 33, ambayo ni mawili pungufu ya yale yaliyoripotiwa mwaka 2021. Asilimia 94 ya wahanga walikuwa ni wanawake, na matukio mengi yaliropotiwa (asilimia 52) yalisababishwa na wivu wa kimapenzi.




> *'..Dada yangu tumemzika mwaka huu mwezi wa pili alipigwa na mme wake hadi akauawa kwasababu alikuwa akimtuhumu mara kwa mara kwamba hazai.'*
>
> **Mwanajamii, Njombe**

### *Matukio mengine ya ukatili wa kimwili na kisaikolojia dhidi ya wanawake*

LHRC ilikusanya matukio mengine ya ukatili wa kimwili na kisaikolojia takribani 73, ikiwemo ukatili wa kimwili unaofanywa na mwenza, kupitia programu ya ufuatiliaji wa haki za

binadamu na utafiti wa taarifa za vyombo vya habari. Matukio haya yaliripotiwa katika mikoa kama vile Dar es Salaam, Songwe, Iringa, Mara, Mwanza, Mtwara, Manyara, Rukwa, na Kilimanjaro. Matukio ya ukatili yaliyoripotiwa ni pamoja na vipigo, kukatwa sehemu za mwili, kushambuliwa na panga, kung'atwa masikio, kupigwa na nyundo, kuingiziwa kitu chenye ncha kali kwenye sehemu za siri, na kufanyiwa ukeketaji.

Pia, LHRC ilikusanya matukio mengine 635 kupitia Utafiti wa Haki za Binadamu wa mwaka 2022, uliofanyika katika mikoa 20 ya Tanzania Bara. Matukio hayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Morogoro, Tabora, Singida, Kagera, Geita, Kigoma, Kilimanjaro, Arusha, na Katavi.

### *Ukatili wa kingono*

Kupitia programu ya ufuatialiaji wa haki za binadamu na utafiti wa taarifa za vyombo vya habari, LHRC ilikusanya matukio 30 ya ukatili wa kingono dhidi ya wanawake, ambayo ni asilimia 28 ya matukio yote ya ukatili dhidi ya wanawake yaliyokusanywa. Matukio hayo ni pamoja na ubakaji, unyanyasaji wa kingono, rushwa ya ngono, na ulawiti ndani ya ndoa. LHRC pia ilikusanya matukio mengine 406 ya ukatili wa kingono dhidi ya wanawake kupitia utafiti wa haki za binadanu, ikiwemo ubakaji, ubakaji wa makundi, unyanyasaji wa kingono, na rushwa ya ngono. Matukio ya ubakaji yaliyokusanywa mwaka 2022 ni pamoja na tukio la ubakaji wa mwanamke mwenye ujauzito mkoani Iringa na ubakaji wa mwanamke mzee mwenye miaka 80, mkazi wa Kijiji cha Mawengi mkoani Njombe.

Ulawiti ndani ya ndoa uliripotiwa pia kama changamoto mwaka 2022. Mathalani, mkoani Dar es Salaam, Joyce Maketa, afisa ustawi wa jamii, alisema kwamba ulawiti ndani ya ndoa ni mojawapo ya sababu za wanawake kudai talaka jijini humo. Maafisa ustawi, maafisa maendeleo ya jamii, viongozi wa dini, na wanajamii wengine katika Mikoa ya Singida, Kilimanjaro, Mbeya, na Katavi, pia walitambua ulawiti ndani ya ndoa kama tatizo.

> *'Kuna kesi zaidi ya tatu za wanaume kuwalazimisha wake zao kushiriki tendo la ndoa kinyume na maumbile na wakikataa wanapigwa, kuna wanaume wawili baada ya kukaa nao wamejirekebisha lakini mmoja ndoa yake imevunjika kutokana na kuendeleza tabia hiyo.'*
>
> **Msaidizi wa kisheria, Halmashauri Jiji Mbeya – Mbeya**

### *Ukatili wa kiuchumi*

Mwaka 2022 LHRC ilikusanya matukio 17 ya ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanawake

kupitia utafiti wa taarifa za vyombo vya habari na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu. Matukio hayo ni pamoja na kunyimwa urithi, kunyang'anywa mali, na kuzuiwa matumizi ya kipato cha familia. Pia, LHRC ilikusanya matukio mengine 350 ya aina hii ya ukatili dhidi ya wanawake kupitia utafiti wake wa haki za binadamu.

Kwa mwaka 2022 LHRC ilikusanya matukio takribani 21 ya wajane kufukuzwa nyumbani kupitia programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu na utafiti wa haki za binadamu, ambayo ni matukio mawili pungufu ya yale yaliyoripotiwa mwaka 2021.

**Wito wa LHRC:** Wanawake na wanaume kuandika wosia kama njia ya kulinda haki za kumiliki mali na urithi, ikiwemo za wanawake na watoto.

### *Ukatili dhidi ya wanawake wanasiasa*

Ukatili dhidi ya wanawake wanasiasa umetafsiriwa kama kitendo chochote cha ukatili wa kimwili, kingono, au kisaikolojia, kinachowazuia wanawake kufurahia na kutekeleza haki zao za kisiasa na haki mbalimbali nyingine za binadamu. Wahanga wa aina hii ya ukatili ni pamoja na wanawake viongozi wa kisiasa, wagombea na watia nia wa kike, washabiki wa kisiasa, wapiga kura, wafanyakazi na waangalizi wa uchaguzi, maafisa wa umma, na watumishi wa serikali. Utafiti wa haki za binadamu uliofanywa na LHRC mwaka 2022 uliangazia pia suala la ukatili dhidi ya wanawake wanasiasa, ambapo asilimia 94 ya wanawake wanasiasa waliohojiwa walikiri kwamba aina hii ya ukatili ni tatizo kubwa katika jamii. Karibia washiriki wote pia waliutaja ukatili wa kingono kama aina kuu ya ukatilil dhidi ya wanawake wanasiasa unaotokea zaidi. Wahojiwa wengi pia walisema vitendo vya rushwa ndiyo changamoto kubwa zaidi inayowakabili wanawake wanasiasa. Baadhi yao pia walisema kuna baadhi ya wanawake pia wanaahidi rushwa ya ngono kwa viongozi wa chama kama watawasaidia kupata uteuzi au kushinda uchaguzi. Wafanyaji wa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake wanasiasa pia hutumia mbinu ya kumchafua mtia nia au mgombea wa kike. Vitisho na uchafuaji wa sifa ya mtu ni miongoni mwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake wanasiasa ambavyo vilidaiwa kutokea zaidi, hasa katika Mikoa ya Tabora, Arusha, Singida, Geita, Kigoma, Katavi, na Tanga.

> *'Siasa ni ngumu sana kwa mwanamke hapa nchini. Tena chaguzi za ndani ya vyama, usijaribu. Mtu anakupendekeza jina na kukuhangaikia upate uongozi na baadaye anakuja kukudai penzi kama malipo yake..'*
>
> **Mwanasiasa mwanamke, Halmashauri Wilaya Mtwara – Mtwara**

*‘Kama ukatili kwa wanawake utaendelea kwenye siasa ina maana wanaume wataendelea kuwa wengi kwenye siasa na wanawake wachache..’*

**Mwanamke mwanasiasa, Nyang’hwale – Geita**

## *Visababishi vya ukatili dhidi ya wanawake*

Visababishi vikuu vya ukatili dhidi ya wanawake ni pamoja na kukubalika kwa ukatili wa kimwili katika jamii na kuonekana ni jambo la kawaida; umaskini na wanawake kutoweza kujitegemea kiuchumi; imani za kishirikina; na mila na tamaduni. Ukatili dhidi ya mwenza hutokea zaidi katika jamii ambayo ukatili dhidi ya wanawake unaonekana ni jambo la kawaida.Karibia nusu ya Watanzania (asilimia 49) wanaamini kwamba mume anastahili kumpiga mke wake kama ameunguza chakula (asilimia 13), akitoka nyumbani bila ruhusua (asilimia 29), akiwatelekeza watoto (asilimia 39), au akibishana naye (asilimia 37). Takribani asilimia 59 pia wanaamini kwamba ni sawa kwa mume kumpiga mke wake akigundua siyo mwaminifu katika ndoa.

*‘Wapo wanawake wanapigwa ila hawaji kutoa taaarifa kwa usatawi wa jamii wala hawaendi dawati la jinsia la polisi. Ukijaribu kuwauliza kwa nini wanaumizwa na hawasemi popote wanasema kuwa wanaona ni jambo la kawaida kwani tangu wakiwa wadogo wamezoea kuona wanawake wanapigwa.’*

**Afisa ustawi jamii, Chato - Geita**

## *Ushiriki wa wanawake katika siasa*

Kwa mwaka 2022, ushiriki wa wanawake katika siasa uliendelea kuathiriwa na vikwazo kadhaa, ikiwemo mianya ya kijinsia katika sheria za uchaguzi, ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; ukatili dhidi ya wanawake wanasiasa; na wanawake wanasiasa kutopewa msaada na ushirikiano wa kutosha ndani ya vyama vya siasa, sambamba na kutokuwa na uwakilishi mzuri katika vyombo vya ufanyaji maamuzi. Kikos kazi cha Rais cha kukusanya maoni kuhusu demokrasia ya vyama vingi nchini Tanzania, kikiongozwa na Prof. Rwekaza Mukandala, kilitoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa kuweka takwa kwa vyama hivyo kutengeneza sera ya jinsia na ushirikishwaji.

## *Uwezeshaji wanawake kiuchumi*

Programu mbalimbali za uwezeshaji wanawake kiuchumi, ikiwemo ile ya kutoa asilimia 4 ya mikopo inayotolewa na

halmashauri kwa wanawake, ziliendelea kuwanufaisha wanawake katika maeneo mbalimbail nchini Tanzania. Hili liliwezekana kwa namna mbalimbali, ikiwemo kuongeza kipato cha familia, kuboresha hali ya maisha, na kupanua biashara. Hata hivyo, bado kuna changamoto kadhaa ambazo zinaathiri programu ya utoaji wa mikopo ya asilimia 4 kwa wanawake, ikiwemo kutorejeshwa kwa mikopo au kasi ndogo ya urejeshaji wa mikopo na uingiliaji wa kisiasa katika mchakato wa utoaji mikopo.

> *'Mpango wa kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ni mzuri sana kwani umesaidia kuwainua wananchi na kuwakwamua kiuchumi, japokuwa kuna changamoto kidogo kwenye urejeshaji wa mikopo hiyo,.'*
>
> **Afisa Maendeleo ya Jamii, Halmashauri Wilaya Geita – Geita**

## *Ulinzi na usalama wa wanawake*


Kwa mujibu wa Ripoti ya Taasisi za Kijamii na Jinsia Tanzania (SIGI), wanawake wengi zaidi kuliko wanaume wanaogopa kutembea peke yao usiku katika maeneo wanayoishi kwa sababu ya hofu ya kufanyiwa ukatili. Asilimia 45 ya wanawake walisema wanaogopa kushambuliwa, kuibiwa, kutekwa, kubakwa, kunyanyaswa kingono, kutukanwa matusi na kutolewa maneno machafu, na kuonyeshwa sehemu za siri. Miongoni mwao, asilimia 33 walisema wanaogopa kuvamiwa na kuibiwa, asilimia 28 walisema wanaogpoa kushambuliwa, na robo (asilimia 25) walisema wanaogopa kubakwa. Pia, LHRC iligundua kwamba kuna wanawake wanashambuliwa na wakati mwingine kuuwawa kwa sababu ya mali, na wengine sababu ya imani za kishirikina, , mfano mkoani Singida, ambapo iliripotiwa kwamba kuna maiti za wanawake zilifukuliwa na kukatwa matiti na sehemu za siri.

**Wito wa LHRC:** Kuna haja ya kuimarisha uwezo wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto ili kuongeza ulinzi wa haki zao, ikiwemo haki ya kuwa salama, uhuru dhidi ya ukatili, na uhuru wa mtu kwenda atakako.

## *Upatikanaji wa haki kwa wanawake*

Kama ilivyokuwa katika nchi nyingi barani Afrika, ubaguzi dhidi ya wanawake nchini Tanzania upo hadi kwenye upatikanaji wa haki. Kwa mujibu wa ripoti ya SIGI ya mwaka 2022, Tanzania ilipata alama 29 pekee katika kiashiria cha "upatikanaji wa haki," huku Mkoa wa Songwe ukionekana kuwa na kiwango cha chini zaidi cha ubaguzi dhidi ya wanawake katika upatikanaji wa haki, kwa kupata alama 13. Mikoa iliyoongoza kwa ubaguzi dhidi ya wanawake katika upatikanaji wa haki ni Iringa, Mwanza, na

Tabora. Ripoti ya SIGI pia inaonyesha uwezo na utayari mdogo wa wanawake kuvifikia vyombo vya polisi na mahakama. Ni asilimia 20 pekee ya wanawake walisema huenda kwenye mahakama ya  chini (Mahakama ya Mwanzo) na robo (asilimia 25) huenda polisi kuomba msaada pale ambapo umetokea mgogoro. Kwa ujumla, uwezekano wa wanaume na wanawake wanaoishi mjini kwenda mahakamani au polisi kutafuta utatuzi wa mgogoro ni mkubwa zaidi kuliko wa wenzao wanaoishi vijijini. Ripoti hiyo pia inaonyesha kwamba wanawake wengi wanapendelea zaidi kutafuta haki au kutatua mgogoro kupitia familia na marafiki.




*Asilimia ya wanawake ambao wanapendelea kuwenda polisi au kwa familia na marafiki unapotokea mgogoro*
*Chanzo: Ripoti ya SIGI Tanzania, 2022*

Hali kadhalika, Ripoti ya SIGI inaonyesha kwamba watu wengi wanaamini kwamba wanaume na wanawake wanatikiwa kuwa na fursa sawa ya kufungua malalamiko polisi. Hata hivyo, zaidi ya theluti tatu walisema kwamba mwanamke anahitaji ruhusa ya mume au mwenza wake kabla ya kwenda polisi (asilimia 77) au mahakamani (asilimia 83). Haya yalikuwa maoni ya zaidi ya asilimia 50 ya wahojiwa katika mikoa yote iliyofanyiwa utafiti.

## 5.2. Haki za Watoto


Haki za watoto zinalindwa katika mikataba mikubwa miwili ya haki za watoto, ambayo ni: Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (CRC) wa mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) wa mwaka 1990, yote ikiwa imeridhiwa na Tanzania. Kwa hapa nchini Tanzania pia tuna Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo inataja haki za msingi za mtoto kama zilivyoelezewa kwenye mikataba hiyo na kueleza wazi kwamba katika kufanya maamuzi yoyote kuhusu mtoto kanuni ya maslahi bora ya mtoto lazima izingatiwe. Mikataba hii na sheria ya mtoto inatoa wajibu kwa Serikali, wazazi, walezi na wanajamii kwa ujumla kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili na ubaguzi.

### *Mienendo na matukio ya ukatili dhidi ya watoto*

Kwa mwaka 2022, masuala makuu yaliyoathiri haki za watoto ni pamoja na: ukatili wa kingono; ukatili wa kimwili na

kisaikolojia; ajira kwa watoto na utumikishwaji wa watoto; ndoa za utotoni; na mimba za utotoni; Ukatili dhidi ya watoto uliendelea kuwa tishio kubwa kwa haki na ustawi wa watoto.


Takwimu za polisi kuhusu ukatili dhidi ya watoto za kipindi cha miaka ya 2017 hadi 2021 zinaonyesha kwamba jumla ya matukio 70,997 ya ukatili dhidi ya watoto yaliripotiwa katika vituo mbalimbali vya polisi, ambayo ni wastani wa matukio 14,199 kila mwaka, matukio 1,183 kila mwenzi, na matukio 39 kila siku.




*Wahanga wa ukatili dhidi ya watoto nchini Tanzania kwa jinsi – 2018 hadi 2021*
*Chanzo: Data za polisi, 2018 hadi 2021*

Kwa mwaka 2022, taarifa za Jeshi la Polisi na viongozi wa Serikali zilionyesha kuongezeka kwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto, ikiwemo ukatili wa kingono, katika mikoa mbalimbali. Haya yalibainishwa zaidi wakati wa maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia zilizofanyika mwezi Disemba mwaka 2022 katika maeneo mbalimbali nchini.

Kupitia utafiti wa taarifa za vyombo vya habari na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu, LHRC ilikusanya takribani matukio 350 ya ukatili dhidi ya watoto mwaka 2022, ambayo yaliripotiwa katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara. Matukio mengi yaliyoripotiwa (asilimia 81) yalikuwa ni ya ukatili wa kingono, yakifuatiwa na ya ukatili wa kimwili na kihisia (asilimia 18). Robo ya wahanga (asilimia 25) walikuwa wana umri wa chini ya miaka 10 na zaidi ya theluthi mbili ya wahanga wa ulawiti (asilimia 78) walikuwa ni wavulana.




*Asilimia ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2022 kwa aina ya ukatili*

Uchambuzi wa matukio ya ukatili dhidi ya watoto ulionyesha kwamba wafanyaji wa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ni pamoja

na baba, mtu asiyejulikana (mwenyeji wa eneo fulani), mzee, ndugu au rafiki wa karibu, mtoto shuleni (hasa kwa suala la ulawiti), mfanyakazi katika sekta ya afya, mwalimu, na dereva bodaboda. Akinababa 14, ndugu wa karibu 30, walimu 10, na viongozi 2 wa kidini (padri 1, ustadhi/mwalimu wa madrasa 1) walitajwa kama wafanyaji wa ukatili wa kingono katika matukio yaliyokusanywa na LHRC.

Wahanga 88 wa matukio ya ukatili dhidi ya watoto (asilimia 25) walikuwa wana umri wa chini ya miaka 10, na wahanga wengine 88 (asilimia 25) walikuwa wahanga wa ukatili dhidi ya watoto unaofanywa na watoto wenzao (watuhumiwa wakiwa na umri wa miaka 14 hadi 17), na wahanga 212 walilawitiwa. Miongoni mwa wahanga wa ulawiti, wavulana walikuwa wengi zaidi, 166 (asilimia 78). Matukio mengi ya ulawiti yaliripotiwa shuleni na nyumbani.

## Mitazamo ya wanajamii kuhusu ukatili dhidi ya watoto

Zaidi kidogo ya nusu ya wanajamii walioshiriki katika utafiti (asilimia 51) walisema ukatili dhidi ya watoto ni tatizo kubwa katika jamii, wakifuatiwa na zaidi kidogo ya robo (asilimia 27), waliosema kwamba ni tatizo, na asilimia 20 waliodai ni tatizo kiasi. Wahojiwa wengi, wakiwemo maafisa ustawi wa jamii, pia walionyesha wasiwasi kuhusu kuongezeka kwa matukio ya ubakaji na ulawiti wa watoto.




*Asilimia ya majibu ya wanajamii kuhusu ukubwa wa tatizo la ukatili dhidi ya watoto (N=1,497)*
*Chanzo: Data za utafiti, 2022*

## Ukatili wa kingono

Ukatili wa kingono ulikuwa ndiyo aina ya ukatili dhidi ya watoto iliyoripotiwa zaidi mwaka 2022, ambapo zaidi ya asilimia 80 ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyokusanywa na LHRC yalikuwa ni ya ukatili wa kingono. LHRC ilikusanya jumla ya matukio 283 ya aina hii ya ukatili dhidi ya watoto kupitia utafiti wa taarifa za vyombo vya habari na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu mwaka 2022.Matukio mengi yalikuwa ni ya ubakaji na ulawiti, na watuhumiwa walikuwa ni pamoja na baba, baba wa kambo, mtu asiyejulikana, mjomba, mzee, ndugu au rafiki wa familia, mtoto shuleni, mfanyakazi katika sekta ya afya, mwalimu, na dereva bodaboda.

Zaidi ya matukio 5000 ya ubakaji na 1000 ya ulawiti yameripotiwa na vyanzo mbalimbali vya Serikali katika miaka ya 2021 na 2022, sawa na wastani wa matukio zaidi ya 400 ya ubakaji na 93 ya ulawiti kila mwezi.

**Wasiwasi kuhusu ulawiti wa watoto:** Maafisa ustawi wa jamii, maafisa maendeleo ya jamii, wasaidizi wa kisheria, na wafanyakazi wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika mikoa mbalimbali iliyotembelewa mwaka 2022 walielezea wasiwasi wao kuhusu matukio ya ulawiti. Walidai matukio haya kutokea zaidi shuleni, yakifanywa na watoto dhidi ya watoto wengine, huku walimu wakidai kwamba hilo ni tatizo katika shule mbalimbali.

> ***'...watoto wanafanyiana ukatili wa kingono wao kwa wao hasa kulawitiana katika maeneo mbalimbali kama mashuleni, njiani wanaporudi majumban,i na hata mazingira ya sehemu wanazoishi..'***
>
> **Mwalimu shule ya msingi – Halmashauri Wilaya Geita, Geita**

> ***'Ulawiti umekithiri hasa kwenye hosteli,wanafanyiana wenyewe kwa wenyewe watoto,sasa hivi ni kuwa nao makini kujua mtoto wako anacheza na nani, utandawazi umeharibu watoto.'***
>
> **Msaidizi wa kisheria – Halmashauri Wilaya Singida, Singida**

**Changamoto ya ukatili dhidi ya watoto unaofanywa na watoto wenzao, hasa katika maeneo ya shule:** LHRC imebaini kwamba tabia ya watoto, hasa watoto wakubwa, kuwafanyia watoto wenzao ukatili wa kingono imeanza kushamiri. Kupitia utafiti wa taarifa za vyombo vya habari na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu, LHRC ilikusanya matukio 88 ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto uliofanywa na watoto wenzao, sawa na asilimia 25 ya matukio ya ukatili wa kiongono yaliyokusanywa. Vitendo hivyo vilifanywa na watoto wenye umri wenye miaka kati ya 14 hadi 17.

**Ukatili wa kingono dhidi ya wavulana:** Tafiti mbalimbali zimebaini kwamba nchi nyingi duniani zimekuwa haziweki mkazo katika kuwalinda kisheria watoto wa kiume, na mara nyingi wavulana wamekuwa hawaangaliwi kama wahanga wa ukatili wa kingono katika jamii. Hii inatokana na imani katika jamii kwamba mtoto wa kiume yuko imara zaidi.

Nchini Tanzania, watoto wa kiume wamekuwa wakifanyiwa zaidi vitendo vya ulawiti, suala ambalo linaonekana kukua mwaka hadi mwaka. Vitendo hivi vinafanyika zaidi katika maenoe ya shuleni na nyumbani. Katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2021 pekee, jumla ya matukio 5,716 ya ulawiti wa watoto yaliripotiwa katika vituo mbalimbali

vya polisi, sawa na wastani wa matukio 900 kila mwaka, 79 kila mwezi, na takribani 2 kila siku. Wahanga wengi (asilimia 87) ni wavulana.




Kwa mwaka 2021, LHRC ilikusanya matukio 34 pekee ya ulawiti wa watoto, japo haya huwa ni machache sana ukilinganisha na yanayoripotiwa polisi. Kwa mwaka 2022, idadi ya matukio yaliyokusanywa na LHRC ilipanda hadi kufikia matukio 166, sawa na asilimia 78 ya matukio yote ya ulawiti yaliyokusanywa. Mnamo mwezi Disemba 2022, iliripotiwa kwamba zaidi ya matukio 1,000 ya ulawiti wa watoto yaliripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2022 pekee, ambayo wavulana walikuwa ni asilimia 84 ya wahanga.

*'Zamani tulikua na hofu zaidi juu ya watoto wa kike, lakini kwa hali ya sasa watoto wa kiume wapo zaidi hatarini kuliko wa kike. Sina uthibitisho wa moja kwa moja wa kisayansi lakini wingi wa matukio ya ulawiti wa watoto mengi yamekua yakifanywa kwa watoto wa kiume ambao wanaharibikiwa zaidi kwa haraka..'*

**Mkurugenzi, Sauti ya Jamii – Iringa**

**Ukatili wa kingono dhidi ya watoto katika taasisi za kidini:** Katika sehemu mbalimbali duniani, ukatili wa kingono dhidi ya watoto umekuwa pia ukiripotiwa kutokea katika taasisi za kidini, ikwemo kanisani na msikitini au madrasa. Changamoto kubwa katika mapambano dhidi ya aina hii ya ukatili katika nchi mbalimbali duniani ni usiri mkubwa na utetezi ambao viongozi au wafanyakazi wanaofanya ukatili huo dhidi ya watoto katika taasisi hizo wanapata. Watuhumiwa wa vitendo hivyo wanatambua kwamba uwezekano wa wahanga kuaminiwa zaidi kuliko wao ni mdogo.

Katika kipindi cha miaka mitano liyopita (2017 – 2021), LHRC ilikusanya takribani matukio tisa ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto katika taasisi za kidini. Hali kadhalika, katika kipindi hicho, LHRC pia ilikusanya matukio mengine 16 yaliyowahusisha viongozi au wafanyakazi katika taasisi za

kidini, ambao walituhumiwa kuwafanyia ukatili wa kingono watoto nje ya taasisi hizo, ikiwemo nyumbani. Hii inaonyesha kwamba kuna uwezekano wa kutokea matukio mengi zaidi ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto katika taasisi za kidini lakini hayaripotiwi au kugundulika mapema kwa sababu ya usiri uliopo na uoga wa kuripoti matukio hayo miongoni mwa wahanga kwa hofu ya kutoaminika.

### *Ukatili wa kimwili dhidi ya watoto*

Asilimia 18 ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2022 kupitia utafiti wa taarifa za vyombo vya habari na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadmu yalikuwa ni ya ukatili wa kimwili na kisaikolojia.Vitendo vya ukatili huu vilivyoripotiwa ni pamoja na kupigwa, kunyongwa, kuchomwa mikono, kuchomwa moto, mtoto kuzikwa akiwa hai, kunyweshwa sumu, na kushambuliwa na silaha. Wazazi ndiyo walituhumiwa zaidi kufanya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Miongoni mwa matukio hayo ni tukio la mtoto mwenye miaka 15 mkoani Arusha, ambaye alishambuliwa na kujeruhiwa vibaya na mume wake pamoja na rafiki wa mume huyo.




*Mtoto mwenye miaka 15 ambaye aliripotiwa kushambuliwa na mume wake pamoja na rafiki wa mume wake Longido mkoani Arusha Picha kwa hisani ya: Jamii Forums (Sep 2022)*

Baadhi ya wazazi katika maeneo mbalimbali Tanzania Bara walituhumiwa kuwapatia watoto adhabu ya kikatili ya kuwachoma mikono na sehemu nyingine za miili yao. LHRC ilikusanya matukio ya aina hii takribani nane, yalilyoripotiwa katika mikoa ya Simiyu, Mtwara, Njombe, Geita, na Kilimanjaro.

Kupitia Utafiti wa Haki za Binadamu wa mwaka 2022, LHRC pia ilikusanya takribani matukio 460 ya ukatili wa kimwili dhidi ya watoto, ambayo yaliripotiwa katika mikoa 7 kati ya 20 iliyotembelewa pekee, ambayo ni Singida, Iringa, Njombe, Kagera, Geita, Kigoma, na Katavi.



*Msichana mkoani Geita ambaye alishindwa kufanya mitihani yake ya darasa la saba baada ya mama yake kumchoma mikono kwa tuhuma za kuiba Sh. 500*
*Chanzo: Data za utafiti, 2022*

## Utelekezaji wa watoto

Utelekezaji wa watoto, ambao unakatazwa katika Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, uliendelea kuwa changamoto kubwa katika ufurahiaji na utekelezaji wa haki za watoto. Kwa mwaka 2022, LHRC ilikusanya matukio 67 ya utelekezaji wa watoto, yaliyoripotiwa katika Mikoa ya Tanga, Lindi, Mtwara, Kilimanjaro, Tabora, Geita, na Simiyu, ambayo ni matukio 43 zaidi ya yale yaliyoripotiwa mwaka 2021. LHRC pia ilikusanya matukio zaidi ya 700 ya utelekezaji wa watoto kupitia utafiti wa haki za binadamu uliofanyika katika mikoa 20 ya Tanzania Bara.

## Ajira kwa watoto na utumikishwaji wa watoto

Kupitia progamu yake ya ufuatiliaji wa haki za binadamu, LHRC ilikusanya matukio 10 ya ajira kwa watoto, yaliyoripotiwa katika Mikoa ya Mbeya, Geita, na Shinyanga. Watoto wengi walisemekana na kukutwa wakifanya kazi katika migodi na mashamba. LHRC ilikusanya matukio mengine 53 ya ajira kwa watoto kupitia utafiti wa haki za binadamu.

## Ndoa za utotoni

Wadaau mbalimbali wa haki za watoto waliendelea kutoa wito kwa Serikali kufanya marekebisho ya sheria kukataza ndoa za utotoni mwaka 2022. Hata hivyo, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 bado haijafanyiwa marekebisho ili kuondoa vifungu vinavyoruhusu ndoa za utotoni kwa kuweka umri wa chini wa kuoa na kuolewa kuwa miaka 18 kwa wanaume na wanawake, kama iliyoelekezwa na Mahakama ya Rufani katika hukumu ya Kesi ya Rebecca Gyumi ya mwaka 2019. Kwa mwaka 2022, LHRC ilikusanya matukio 16 ya ndoa za utotoni kupitia utatifi wa taarifa za vyombo vya habari na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu, yakipungua kutoka matukio 37 mwaka 2021. Mwaka 2022 iliripotiwa katika baadhi ya mikoa kwamba baadhi ya wazazi walikuwa wakiwaambia watoto wao wa kike

wafeli kwa makusudi mitihani yao ya taifa ili wakaolewe. Baadhi ya visababishi vikuu vya ndoa za utotoni vilivyotajwa ni pamoja na kukubalika kwa ndoa hizo na suala zima la mahari.



*Wasichana wawili waliookolewa na polisi kutoka kwenye ndoa za utotoni mkoani Katavi (kushoto) na ng'ombe waliokuwa wametolewa kama mahari (kulia)*
*Chanzo: Data za utafiti, 2022*


## *Mimba za utotoni*

Kwa mwaka 2022, matukio ya mimba za utotoni yaliendelea kuripotiwa katika mikoa mbalimbali Tanzania Bara. Kupitia utafiti wa vyombo vya habari na programu ya ufuatiliaji wa haki za binadamu, LHRC ilikusanya zaidi ya matukio 6,000 ya mimba za utotoni, yaliyoripotiwa katika mikoa mbalimbali, ikiwemo Kigoma, Pwani, Mwanza, Katavi, Rukwa, na Arusha.

Mnamo tarehe 15 Septemba 2022, Kamati ya Afrika ya Wataalamu wa Haki za Watoto ilitoa maamuzi yake katika kesi ya kuwapima ujauzito kinguvu na kuwafukuza shuleni wasichana wenye mimba na walioolewa, iliyofunguliwa na LHRC pamoja na shirika lingine lililopo Afrika Kusini. Kamati iliamua kwamba kwa kuchukua hatua hizo, Tanzania ilikiuka haki mbalimbali za wasichana zinazotambuliwa na kulindwa katika Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto. Haki hizo ni pamoja na ulinzi dhidi ya utesaji na kutendewa kama siyo binadamu; haki ya elimu; haki ya kutobaguliwa; ulinzi dhidi ya desturi zenye madhara; haki ya faragha; na haki ya afya. Kamati pia ilisema hatua hizo zilikiuka kanuni ya maslahi bora ya mtoto.

Hali kadhalika, matokeo ya awali ya Utafiti wa Kidemografia na Afya na Utafiti wa Viashiria vya Malaria wa mwaka 2022 yalionyesha kwamba asilimia 22 ya wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 19 wamewahi kupata mimba, asilimia 16 walijifungua salama, asilimia 2 walipoteza ujauzito, na asilimia 6 wana ujauzito kwa sasa. Asilimia ya wanawake wenye miaka 15 hadi 19 ambao wamewahi kuwa na ujauzito ni kubwa zaidi katika maeneo ya vijijini (asilimia 24.9) ukilinganisha na mijini

(asilimia 16.4). Kimkoa, asilimia kubwa zaidi ya wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 19 waliowahi kupata mimba ilikuwa ni katika Mkoa wa Songwe (asilimia 44.7), ukifuatiwa na Ruvuma (asilimia 37.2).




*Asilimia ya wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 19 waliowahi kupata ujauzito*
*Chanzo:TDHS – MIS 2022 & uchambuzi wa mwandishi*

### *Usafirishaji haramu wa watoto*

Katika miaka ya hivi karibuni, usafirishaji haramu wa watoto umeendelea kuwa changamoto katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania, hasa usafirishaji kwa ajili ya kuwatumikisha watoto kikazi na kingono. Matukio nane kati ya kumi na mbili ya usafirishaji haramu wa binadamu yaliyokusanywa na LHRC kupitia utafiti wa tarifa za vyombo vya habari na program ya ufuatiliaji wa haki za binadamu yalikuwa ni ya usafirishaji haramu wa watoto. Kupitia utafiti wa haki za binadamu, LHRC pia ilikusanya matukio 62 ya usafirishaji haramu wa watoto, yaliyoripotiwa katika mikoa kama vile Singida, Njombe, na Dar es Salaam. Afisa ustawi wa jamii mmoja mkoani Singida alidai kwamba kuna watoto mkoani humo ambao wamekuwa wakisafirishwa kiharamu kwa ajili ya kutumikishwa majumbani na kingono.

## 5.3. Haki za Watu wenye Ulemavu

Masuala makuu yaliyoathiri haki za watu wenye ulemavu kwa mwaka 2022 ni pamoja na ukuzaji na ulinzi wa haki zao; upatikanaji wa ajira na fursa za kiuchumi, ikiwemo ubaguzi katika ajira; unyanyapaa na ubaguzi, ikiwemo ubaguzi dhidi ya watoto wenye ulemavu; aina tofauti za ukatili, hasa ukatili wa kimwili; na upatikanaji wa huduma za afya; na ukosekanaji wa miundombinu rafiki.

### *Unyanyapaa na ubaguzi*

Kwa mwaka 2022, matukio ya unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu yaliripotiwa katika mikoa kama vile Njombe, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Katavi, Rukwa, Mbeya, Iringa, na Morogoro. Mojawapo ya changamoto kuu ambayo watu wenye ulemavu walikumbana nayo

ni kutengwa katika familia na jamiii, hasa watoto wenye ulemavu.

> *''Ndugu mtaalamu watoto wengi wenye ulemavu wanafungiwa ndani na wazazi wao na wengine sio rahisi kuonekana mpaka uwe mtu wa karibu kabisa ndio utajua...inabaki kuwa siri ya familia hawa watoto wengi hawapelekwi shule na wala hawatolewi nje ili kuficha aibu ya ulemavu sababu ulemavu pia unachukuliwa kuwa ni laana'*
>
> **Mtu mwenye ulemavu – Ludewa, Njombe**

### *Ubaguzi katika ajira*

Utafiti kuhusu biashara na haki za binadamu uliofanywa na LHRC mwaka 2022 katika mikoa 14 ulionyesha kwamba kuna baadhi ya waajiri katika sekta ya biashara ambao hawapendi kuwaajiri watu wenye ulemavu kwa sababu 'hawana ufanisi kama watu wasio na ulemavu.' Waajiri wengine walisema kwamba hawawaajiri watu wenye ulemavu viwandani kwa sababu 'wanaweza kuchelewesha uzalishaji' na mazingira 'siyo rafiki' kwao.

### *Ukatili*

Katika kipindi cha mwaka 2022, LHRC ilikusanya takribani matukio 12 ya ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu, ikiwemo vitendo vya ukatili dhidi ya watu wenye ualbino na watoto wenye ulemavu. Vitendo hivyo vya ukatili ni pamoja na ubakaji, shambulio la mwili, matusi, kutengwa, na kunyimwa haki ya elimu.

Matukio ya shambulio na mauaji ya watu wenye ualbino yameanza kuibuka upya miaka ya hivi karibuni. Mathalani, mwaka 2021 liliripotiwa tukio la mtoto mwenye ualbino mwenye umri wa miaka 4 hadi 7 kushambuliwa na kuuwawa kule mkoani Tabora. Kwa mwaka 2022, tukio jingine la shambulio na mauaji ya mtu mwenye ualbino liliripotiwa katika Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza, ambapo Joseph Mathias (50), alishambuliwa na watu wasiojulikana na kukatwa mkono, hali iliyosababisha atokwe na damu nyingi na hatimaye kufariki.

### *Upatikanaji wa huduma bora na rafiki za afya*

Mnamo mwezi Machi mwaka 2022, wanawake wenye ulemavu nchini waliiomba Serikali kuboresha huduma za afya na kulisaidia kundi hilo kupata huduma bora za afya, ikiwemo kwa mama na mtoto, kwani suala hilo limekuwa changamoto katika hospitali na vituo mbalimbali vya afya. Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) lilisema pia kwamba Serikali inatakiwa kuingilia kati suala hili kwani wanawake wenye ulemavu wanapata changamoto nyingi wakati wa ujauzito na kujifungua. Shirikisho hilo

liliiomba Serikali kupeleka vitanda maalum kwa ajili ya wanawake wenye ulemavu wajawazito katika hospitali mbalimbali nchini, sambamba na kuweka wataalamu wa lugha ya alama ili kurahisisha mawasiliano kwa sababu wataalamu wengi wa afya hawana uelewa mzuri kuhusu aina mbalimbali za ulemavu.

## 5.4. Haki za Wazee

Tofauti na makundi mengine maalum kama vile wanawake, watoto na watu wenye ulemavu, hakuna mkataba wa kimataifa wa haki za binadamu maalum kwa ajili ya wazee. Kwa hapa nchini hakuna pia sheria ya kuwalinda wazee, japokuwa Zanzibar ipo. Katika Utafiti wa Haki za Binadamu uliofanywa na LHRC mwaka 2021, zaidi ya nusu ya wanajamii walioshiriki katika utafiti huo walidai kwamba haki za wazee zimelindwa kiasi. Hata hivyo baadhi ya wanajamii, wakiwemo wazee, waliohojiwa walisema kwamba wazee wanakabiliana na changamoto mbalimbali, ikiwemo upatikanaji wa huduma bora za afya, ukatili, na kukosa ulinzi/hifadhi ya kijamii.

Kwa mwaka 2022, masuala makuu yaliyoathiri haki za wazee nchini Tanzania ni pamoja na aina tofauti za ukatili, ambazo zilikuwa tishio kwa usalama na ustawi wao; upatikanai wa huduma za afya; mauaji; na ulinzi wa kijamii/hifadhi ya jamii.

### *Ulinzi kwa wazee*

Kwa mwaka 2022, wadau mbalimbali waliendelea kutoa wito wa utungaji wa sheria ya ulinzi wa haki za wazee, ili kuwalinda wazee, kama ilivyofanyika kwa upande wa Zanzibar. Sheria hiyo, pamoja na mambo mengine, itambue haki ya kupata pensheni kwa wazee wote.

Kutokuwepo kwa ulinzi wa kijamii wa kutosha pia kumeendelea kuwa changamoto kubwa kwa wazee. Kwa mujibu wa shirika linalojishughulisha na wazee la HelpAge International, ni asilimia 4 wazee pekee nchini Tanzania wana pata pensheni, jambo linalowafanya walazimike kufanya shughuli ngumu, kwa kuzingatia umri wao, kama vile kilimo, ili kuweza kujikimu.

Mnamo mwezi Septemba mwaka 2022, mashirika ya Shirika la Afya Duniani na shirika linalojihusisha na haki za wazee la HelpAge International yalitoa wito kwa serikali kutunga sheria maalum ambayo isimamia na kuimarisha ulinzi wa haki za wazee nchini Tanzania kwa kuzingatia mahitaji yao yote.

### *Upatikanaji wa huduma bora za afya*

Wazee waliendelea kuathiriwa zaidi na changamoto mbalimbali za upatikanaji

wa huduma bora za afya mwaka 2022. Changamoto hizo ni pamoja na ukosekanaji wa huduma za afya karibu na makazi yao, upungufu wa wafanyakazi katika sekta ya afya, na upungufu wa madawa na vifaa tiba.

### *Ukatili*

LHRC ilikusanya matukio 24 ya ukatili dhidi ya wazee, ambayo yaliongezeka kutoka matukio 16 yaliyokusanywa mwaka 2021. Hata hivyo, hii ni sehemu ndogo tu ya matukio ambayo kwa kawaida huripotiwa polisi, ukizingatia pia kwamba kuna matukio mengi ya ukatili dhidi ya wazee ambayo huwa hayaripotiwi.

Wazee wanawake kwa wanaume walifanyiwa vitendo mbalimbali vya ukatili, ikiwemo ukatili wa kimwili, kingono, kisaikolojia, na kiuchumi. Vitendo hivyo ni pamoja na ubakaji, vipigo, utelekezaji, kushambuliwa na vitu vyenye ncha kali, na kunyang'nywa mali. Matukio ya wazee kushambuilwa na hata kuuliwa yaliripotiwa katika mikoa mbalimbali. LHRC illikusanya takribani matukio nane ya wazee waliouwawa na watoto wao wenyewe, ambayo ni matukio matatu zaidi ya yale yaliyoripotiwa katika miaka ya 2020 na 2021 kwa pamoja. Mathalani, mnamo mwezi Machi 2022, polisi wilayani Nzega walimkamata Michael Jacob (25) kwa kumuua kikatili baba yake kwa tuhuma za uchawi. Mwezi Disemba iliripotiwa kwamba polisi mkoani Njombe walimkamata Otmary Wangerage (38), mkazi wa Mji wa Njombe, kwa kumbaka mwanamke mzee mwenye miaka 80.

> *'Wazee ndio wachawi na ndio wanaomaliza vijana wengi hapa kijijini tukienda kwa waganga na tukaambiwa kwamba mzee fulani ndio kamroga mtu fulani sisi hatujiulizi mara mbili ni kumuondoa tu.'*
> **Mwanajamii (mwanamke) – Halmashauri Wilaya Njombe, Njombe**

## 5.5. Haki za Vijana

Kama ilivyo kwa vijana wengine katika sehemu mbalimbali duniani, barani Afrika vijana pia wana mkataba mahsusi kwa ajili yao, uitwao Mkataba wa Vijana wa Kiafrika wa mwaka 2006. Kwa mujibu wa mkataba huu, kijana ni mtu yeyote mwenye umri wa miaka kati ya 15 na 35.
Kwa mwaka 2022, LHRC ilingundua kwamba masuala makuu yanayowafikirisha vijana Tanzania Bara ni 1. Ajira 2. Ubora wa elimu 3. Afya 4. Ubaguzi & ukatili 5. Ushiriki katika ufanyaji maamuzi.

*'Unakuta mtu ameshafika umri wa kustaafu halafu anarudishwa tena kazini,sasa hawa vijana awaliotoka vyuoni wataajiriwa sangapi?Kuwe kuna ukomo wa kuajiriwa na sisi tuajiriwe.'*

**Kijana – HW ya Singida, Singida**

*'Mimi nimeshakata tamaa na ajira, pamoja na kuwa na sifa nzuri za kuajiriwa kwa sababu nimechoka kuombwa rushwa ya ngono ili nipate kazi au kupitishwa kuitwa kwenye interview. Ni bora nihangaike na biashara mtandaoni, japo bado nina changamoto ya mtaji.'*

**Kijana – HJ la Arusha, Arusha**

Kwa ujumla, vijana waliofikiwa na utafiti wa haki za binadamu uliofanyika katika mikoa 20 ya Tanzania Bara walitaja mambo yafuatayo kama masuala na changamoto kuu:

- Ajira na fursa za kiuchumi.
- Uvivu na uraibu wa mitandao ya kijamii
- Ufahamu wa afya na haki za uzazi.
- Upatikanaji wa huduma bora na rafiki za afya.
- Afya ya akili.
- Desturi za kimila zenye madhara,ikiwemo ukeketaji na ndoa za utotoni na kulazimishwa
- Ushiriki katika siasa, uongozi, na ufanyaji maamuzi.
- Ubora wa elimu.
- Kuwa katika hatari ya kufanya uhalifu, kujiingiza katika ulevi, kutumia madawa, kupata mimba za utotoni, na kujiingiza katika umalaya.

Vijana ambao wako katika vikundi vinavyopewa mkopo wa asilimia 4 na halmashauri, pia walifikiwa na kuulizwa kuhusu programu hiyo ya uwezeshaji vijana kiuchumi. Walitambua mchango wa programu hiyo katika kuinua maisha yao, lakini pia walielezea changamoto mbalimbali, ikiwemo utoaji wa mikopo kwa vikundi visivyo na sifa, matumizi mabaya ya fedha za mkopo, upendeleo, kutopewa stadi za ujasiriamali na uandishi wa andiko mradi, na ucheleweshaji katika utoaji wa mikopo.

## 5.6. Haki za Makundi Mengine Maalum, ikiwemo Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI

Makundi mengine maalum, ikiwemo watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na wakimbizi, pia yalikabiliwa na changamoto kadhaa katika ufurahiaji wa haki zao. Kwa upande wa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, changamoto kubwa ilikuwa ni upatikanaji wa huduma bora za afya, unyanyapaa, na ubaguzi. Wanawake na wasichana wanaathirika zaidi na unyanyapaa na ubaguzi.

Mnamo mwezi Agosti mwaka 2022, iliripotiwa kwamba vita dhidi ya UKIMWI, Malaria, na Kifua Kikuu inaweza kuathiriwa sana na kupungua kwa rasilimali fedha kwa jili ya kupambana na magonjwa hayo katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Hii ni kwa mujibu wa ripoti mpya ya Shirika la Umoja wa Mataifa la UKIMWI. Jambo hili limeleta wasiwasi kuhusiana na upatikanaji wa madawa ya kufubaza virusi vya UKIMWI (ARV) kwa Watanzania milioni 1.7 wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Kwa upande wa wakimbizi, masuala makuu yaliyoripotiwa kuathiri haki zao ni pamoja na ukosefu wa ajira, kutoishi katika hali inayofaa, na ukatili. Mathalani, katika Kambi ya Wakimbizi ya Nduta mkoani Kigoma, iliripotiwa kwamba kuna masuala kadhaa yanayoathiri haki za wakimbizi katika kambi hiyoo, ikiwemo ukatili wa kijiinsia, ambapo iliripotiwa kwamba zaidi ya matukio 1000 ya ukatili wa kijinsia yamekuwa yakiripotiwa kila mwaka. Matukio haya yanafanywa na wakimbizi wenyewe na baadhi ya wanajamii, ambao wamekuwa wakiwavizia wanawake na kuwafanyia vitendo vya ukatili, ikiwemo wakati wanaenda kutafuta kuni. Wakimbizi wa kiume pia walituhumiwa kuwafanyia ukatili wa kiuchumi wakimbizi wa kike, ikiwemo kwa kuwanyang'nya vitu vyao.

06

SURA YA SITA:

# MIFUMO YA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU



SURA YA SITA:

# MIFUMO YA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU

## Utangulizi

Mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu inajumuisha taasisi zinazokuza na kulinda haki za binadamu, ambazo zimeundwa katika ngazi za kitaifa, kikanda, na kimataifa.

## 6.1. Mifumo ya Kitaifa ya Ulinzi wa Haki za Binadamu.

Mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu nchini Tanzania inajumuisha vyombo kama vile Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mhimili wa Mahakama, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Jeshi la Polisi Tanzania, na Jeshi la Magereza.

Pamoja na juhudi mbalimbali za kukuza na kulinda haki za binadamu nchini Tanzania, mifumo hii iliendelea kukabiliwa na chamoto mbalimbali, ikiwemo upungufu wa wafanyakazi; ucheleweshaji katika uchunguzi na ukamilishaji wa kesi; rushwa; mianya katika uwezo wa utendaji kazi, hasa kwa upande wa uchunguzi; mianya katika ufuatiliaji na tathmini; ufinyu wa bajeti; na mazingira duni ya kazi, hasa kwa upande wa polisi.


## 6.2.Mifumo ya Kikanda na Kimataifa ya Ulinzi wa Haki za Binadamu

Masuala makuu yaliyoathiri nafasi ya mifumo ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu katika kulinda haki za binadamu nchini ni pamoja na Tanzania kuondoa ruhusa ya watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kufungua kesi kwa niaba ya watu katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Watu na Binadamu na kutotekelezwa kwa hukumu na mapendekezo ya mifumo hiyo katika kesi mbalimbali zilizofunguliwa dhidi ya Tanzania.

### *Tathmini ya Rekodi ya Tanzania katika ulinzi wa haki za binadamu (UPR) iliyofanywa na Baraza la Umoja wa*

## *Mataifa la Haki za Binadamu mwaka 2021*

Rekodi ya haki za binadamu ya Tanzania ilifanyiwa tathmini (tathmini ya UPR) kwa mara nyingine na Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu mnamo tarehe 5 mwezi Novemba mwaka 2021. Mnamo mwezi Machi mwaka 2022, Kikosi Kazi cha baraza hilo kilitoa ripoti ya matokeo ya tathmini hiyo, ambayo inaonyesha kwamba Tanzania ilikubali mapendekezo 187 (mapendekezo 20 yakikubaliwa kiasi), na ilitambua mapendekezo 65. Asilimia ya mapendekezo yaliyokubaliwa na Tanzania yaliongezeka kutoka asilimia 43 mwaka 2021 hadi asilimia 66 mwaka 2022, huku asilimia ya mapendekezo yaliyotambuliwa ikipungua kutoka asilimia 52 mwaka 2021 hadi asilimia 26 mwaka 2022.




*Asilimia ya mapendekezo ya UPR ambayo Tanzania imeyakubali, kuyakubali kiasi, na kutambua mwaka 2022 kufuatia tathmini ya mwaka 2021 (N=252)*
*Chanzo: Ripoti ya Mchakatao wa UPR ya Kikosi Kazi cha Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu 2022*



07


SURA YA SABA:

# UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO KATIKA RIPOTI ZILIZOPITA

## SURA YA SABA:

# UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO KATIKA RIPOTI ZILIZOPITA

Ripoti za haki za binadamu zinazoandaliwa na LHRC zinatoa mapendekezo ya kuimarisha ukuzaji na ulinzi wa haki za binadamu nchini Tanzania kwa wadau mbalimbali wa kiserikali na wasio wa kiserikali . Utekelezaji wa mapendekezo hayo ni kipimo muhimu katika kujua ni hatua gani tumepiga katika kuimarisha haki za binadamu nchini Tanzania. Kwa mwaka 2022, asilimia ya mapendekezo ambayo yalitekelezwa ilikuwa ni 35, ikiongezeka kutoka asilimia 31 mwaka 2021. Aislimia ya mapendekezo yaliyotekelezwa kiasi pia yaliongezeka kutoka asilimia 37 mwaka 2021 hadi asilmia 38 mwaka 2022, huku ya yale ambayo hayajatekelezwa ikipungua kutoka asilimia 29 mwaka 2021 hadi asilmia 26 mwaka 2022.




*Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti za haki za binadamu za (2015 – 2021)*

Mapendekezo mengi yaliyotolewa (asilimia 47) yalikuwa ni kwa upande wa haki za kiraia na kisiasa. Hii ni kwa sababu haki hizi ndiyo haki nyingi zaidi, kama zilivyoelezewa katika nyaraka mbalimbali za kikanda na kimataifa za haki za binadamu, ikiwemo mikataba. Pia, haki hizi ndizo zinazoongoza kwa kukiukwa ukilinganisha na makundi mengine ya haki

za binadamu. Mapendekezo kuhusu haki za kiraia na kisiasa pia yameongoza kwa upande wa idadi ya mapendekezo yaliyotekelezwa (asilimia 48) na ambayo hayajatekelezwa (asilimia 49).

**Wito wa LHRC:** Ili kuimarisha ulinzi wa haki za msingi za binadamu, usawa wa kijamii, na ufikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, tunaisihi Serikali na wadau wengine kutekeleza mapendekezo ambayo bado hayajatekelezwa na yale ambayo hayajatekelezwa kikamilifu.



08

SURA YA NANE:

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO MUHIMU

SURA YA NANE:

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO MUHIMU

## Hitimisho

### *Haki za Kiraia na Kisiasa*

Kwa mwaka 2022, LHRC iligundua kwamba kuna mambo kadhaa chanya yalitokea katika ukuzaji na ulinzi wa haki za kiraia na kisiasa, ikiwemo kufunguliwa kwa vyombo vinne vya habari vilivyofungiwa mwaka 2016 na 2017, ahadi ya kuondoa katazo la mikutano ya kisiasa, na mipango ya kufanya maboresho ya mfumo wa haki jinai nchini. Mambo haya yalichangia kuimarisha kiasi ulinzi na ukuzaji wa haki za kiraia na kisiasa. Hata hivyo, haki hizi ziliendelea kuwa haki zinazokiukwa zaidi mwaka 2022, kwa sababu mbalimbali kama vile uwepo wa sheria na kanuni zenye vifungu vinavyominya haki kinyume na sheria na viwango vya kimataifa, hasa uhuru wa kujieleza, kukusanyika, na kujumuika; rushwa na ucheleweshaji katika utoaji wa haki; ubaguzi wa kijinsia; aina tofauti za ukatili, ikiwemo ukatili dhidi ya wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, na wazee; kutozingatia utaratibu wa kisheria; ukamataji na uwekaji kuzuizini kinyume na sheria; na mauaji.

### *Haki za Kiuchumi, Kijamii, na Kiutamaduni*

Utekelezaji madhubuti wa haki za kiuchumi na kijamii mwaka 2022 uliendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile ufinyu wa bajeti; upungufu wa wafanyakazi, ikiwemo katika sekta za elimu na afya; upungufu wa madarasa na mabweni; upungufu wa matundu ya vyoo; ukatili dhidi ya watoto; desturi zenye madhara; ukosekanaji wa ulinzi wa kijamii kwa watu wengi; na ukiukwaji wa haki za wafanyakazi. Pamoja na changamoto hizi, hali ya haki za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni illimarika kiasi ukilinganisha na mwaka 2021. Mojawapo ya masuala chanya yaliyoimarisha haki hizi ni pamoja na uletwaji wa Waraka mpya wa Viwango vya Chini vya Mshahara vya mwaka 2022, ambao umeondoa Waraka wa Viwango vya Chini vya Mshahara wa mwaka 2013, na uletwaji

wa muswada wa bima ya afya kwa wote.

### *Haki za Kiujumla*

Masuala mbalimbali kama vile ahadi ya kuondoa katazo la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa na uundwaji wa kikosi kazi cha kuchukua maoni kuhusu demokrasia ya vyama vingi, yalikuwa na athari chanya kwenye haki za kiujumla, hususan haki ya maendeleo. Hata hivyo, bado kuna changamoto katika kuboresha maendeleo ya watu, kwa sababu ya changamoto kama vile rushwa, misamaha ya kodi, ukwepaji kodi, na uchafuzi wa mazingira.

### *Haki za Makundi Maalum*

Makundi maalum ni pamoja na wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, vijana, wakimbizi, wazee, na watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Makundi haya yapo katika hatari zaidi ya kufanyiwa vitendo vya ukiukwjai wa haki za binadamu, hivyo kuhitaji ulinzi maalum katika sheria na mikataba mbalimbali. Kwa mwaka 2022, matukio ya ukatili na ubaguzi dhidi ya makundi maalum yaliripotiwa katika mikoa mbalimbali, na kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na LHRC, matukio haya yaliongezeka ukilinganisha na mwaka 2021. Aina mbalimbali za ukatili, kama vile ukatili wa kingono, kimwili, na kiuchumi, uliendelea kuwa tishio kubwa kwa ufurahiaji madhubuti wa haki za makundi maalum.

## Mapendekezo Muhimu

### *Haki za Kiraia na Kisiasa*

1. Jeshi la Polisi Tanzania kuchukua hatua za haraka kufuatilia matukio ya watu kujichukulia sheria mkononi na mauaji yanayotokana na imani za kishirikina na kuhakikisha kwamba watu wanaofanya matukio hayo wanafikishwa mbele ya vyombo vya sheria.
2. Kwa kuwa Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo hazitekelezi adhabu ya kifo, Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, itangaze rasmi kwamba imesitisha adhabu ya kifo na kufanya marekebisho ya sheria kuondoa adhabu hiyo kwenye sheria.
3. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kuridhia na kupitisha Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Usalama Barabarani wa mwaka 2016.
4. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kufanyia marekebisho Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 kulingana na hukumu ya Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki ya mwaka 2019.
5. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kurekebisha Kanuni za Maudhui ya Mtandaoni ya mwaka 2022 ili

yaendane na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.

6. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Jeshi la Polisi Tanzania kuhakikisha askari polisi katika ngazi zote wanapatiwa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu Kanuni za Umoja wa Mataifa za Matumizi ya Nguvu na Silaha za Moto ya Maafisa wa Vyombo vya Dola na haki za binadamu kwa ujumla, kama sehemu ya juhudi za kupunguza mauaji yanayotokana na maafisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi.
7. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kurekebisha Sheria ya Vyama vya Siasa ili iandane na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.
8. Serikali kuondoa katazo la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa.
9. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kuridhia Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi, na Utawala wa mwaka 2007.
10. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kufanya mabadilko ya kisheria katika mfumo wa haki jinai ili kuondoa changamoto mbalimbali, ikiwemo uwekwaji kizuizini kwa muda mrefu. Sheria iseme wazi ukomo wa uwekwaji kizuizini na hatua gani za kuchukua pale ambapo ukomo huo haujazingatiwa.
11. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kutunga sheria ya uanzishwaji wa chombo huru cha kiraia cha kuangalia utendaji wa maaskari polisi na maafisa wengine wa vyombo vya dola ili kuongeza na kukuza uwajibikaji katika vyombo hivyo.
12. Jeshi la Polisi kuhakikisha askari polisi wanajiepusha na vitendo vya ukamataji na uwekaji kizuizini wa watuhumiwa kinyume na sheria naa kutowapeleka watuhumiwa mahakani ndani ya masaa 24 kama inavyotakiwa kisheria, ili kukuza haki ya kuwa huru.
13. Jeshi la Polisi kuhakikisha askari polisi wanajiepusha na vitendo vya ubambikaji wa kesi na vitendo vingine vinavyokinzana na maadili ya Jeshi la Polisi, na kuhakikisha wale wanaofanya vitendo hivyo wanachukuliwa hatua za kisheria.
14. Jeshi la Polisi Tanzania kuhakikisha dhamana kwa makosa yote yenye dhamana inatolewa kwa wakati, kama inavyotakiwa katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.
15. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kuchukua hatua za kisheria na kiutawala kulinda haki ya kushiriki katika utawala, ikiwemo kuruhusu uwepo wa wagombea binafsi na kuundwa kwa chombo huru .
16. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na

Sheria, kuridhia na kutungia sheria Mkataba dhidi ya Utesaji na Adhabu au Vitendo vingine vya Kikatili, visivyo vya Kibinadamu, vya Kinyama na vyenye Kudhalilisha wa Mwaka 1984 (Mkataba dhidi ya Utesaji) ili kuongeza ulinzi wa uhuru dhidi ya utesaji.

17. Viongozi wa dini na wa kimila kutumia ushawishi na majukwaa yao kukemea ukiukwaji wa haki za kiraia, hasa haki ya kuishi, uhuru wa kujieleza, na uhuru dhidi ya utesaji, kama njia ya kukuza haki hizi.
18. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kufanya mapitio ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ili kufanyia kazi maoni ya wadau.
19. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kushirikiana na asasi za kiraia kueneza uelewa kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi na sheria ya ulinzi wa taarifa hizo.

## Haki za Kiuchumi, Kijamii, na Kiutamaduni

1. Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, kuongeza bajeti inayotengwa kwa ajili ya sekta za elimu, afya, maji, na kilimo, kama inavyotakiwa katika viwango mbalimbali vya kimataifa, na kuhakikisha fedha zinapelekwa wizarani kwa wakati.
2. Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia kuchukua hatua ya kushughulikia changamoto ambazo walimu wanakumbana nazo ili kuhakikisha mazingira ya ufundishaji yanaboreshwa, suala ambalo ni muhimu katika kuongeza ubora wa elimu na kufikia malengo muhimu chini ya Lengo la Maendeleo Endelevu namba 4 na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.
3. Wanajamii kuripoti matukio ya ukiukwaji wa haki za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni kwa mamlaka husika.
4. Bunge la Tanzania kuwashirikisha katika mchakato wa bima ya afya kwa wote wadau mbalimbai wa haki ya afya, ikiwemo asasi za kiraia, na kuzingatia maoni na mapendekezo yao, sambamba na kuzingatia mtazamo wa haki za binadamu.
5. Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, kuongeza bajeti kwa ajili ya miradi ya maji, hasa maeneo ya vijijni, ili kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama, suala ambalo pia ni muhimu katika kukuza sekta ya viwanda.
6. Serikali, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Watu wenye Ulemavu), kuhakikisha utekelezaji Madhubuti wa sheria na kanuni za kazi, hasa katika sekta ya biashara, ili kulinda haki za wafanyakazi.
7. Asasi za kiraia kushirikiana na Ofisi ya

Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Watu wenye Ulemavu) kueneza uelewa wa umma kuhusu sheria za kazi na haki na wajibu wa wafanyakazi mara kwa mara.

8. Wanajamii kutafuta maarifa na taarifa kuhusu haki za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni, ikiwemo haki ya kumiliki mali, kupitia machapisho mbalimbali ya lugha rahisi yanayotolewa na Serikali na wadau wengine, zikwemo asasi za kiraia.
9. Serikali, kupitia Wizara Ardhi, Nyumba,na Maendeleo ya Makazi kuongeza juhudi za kuhakikisha upatikanji wa nyumba bora. Juhudi za pamoja na kisekta pia zinahitajika kushughulikia changamoto mbalimbali za upatikanaji wa nyumba bora.
10. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kufanya maboresho ya kisheria kulinda haki za wanawake na wasichana za kulimiki mali na kuishi katika nyumba bora, ikiwemo kwa kufanya mapitio ya sheria baguzi za urithi na kumiliki mali.
11. Asasi za kiraia kueneza uelewa wa umma haki za chakula na kuishi katika nyumba bora, ikiwemo changamoto zinazohusiana na haki hizo.
12. Seriali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Afya, kuongeza kasi ya mchakato wa kutunga sheria kuhusu bima ya afya kwa wote.
13. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Watu wenye Ulemavu) kuhakikisha sheria za ulinzi wa kijamii zinatekelezwa ipasavyo na waajiri wanapekeka michango ya mifuko ya hifadhi ya jamii.

## Haki za Kiujumla

1. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda, na Biashara, kutumia mtazamo wa haki za binadamu katika uwekezaji wa ndani nan je kwa kuzingatia sheria za nchi na hesima kwa za binadamu.
2. Asasi za kiraia, ikiwemo vyombo vya habari, kueneza uelewa wa umma kuhusu haki za kiujumla, ikiwemo haki ya maendeleo na haki ya kufaidika na rasilimali asilia.
3. Serikali, kupitia Wizara ya Madini, kuongeza juhudi za kupambana na ukwepaji kodi, hasa katika sekta ya madini, na kuhakisha makampuni yanayokwepa kodi yanawajibishwa kisheria.
4. Serikali, Kupitia Baraza la Taifa la Mazingira, kuhakikisha na kusimamia utekelezaji madhubuti wa sheria na kanuni za mazingira ili kulinda haki ya mazingira safi na salama.
5. Makampuni na viwanda kuhakikisha ulinzi wa mazingira katika utekelezaji

wa shughuli zake na kuchukua hatua kupunguza athari za shughuli hizo kwenye mazingira.

## Haki za Makundi Maalum

1. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kupeleka bungeni muswada wa kutunga sheria maalum ya ukatili wa kijinsia/ukatili majumbani.
2. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, Tume ya Kurekebisha Sheria, na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kuhakikisha mabadiliko ya kisheria na kisera yanafanyika ili kuhakikisha ukatili dhidi ya wanawake na watoto mtandaoni yanajumuishwa kwenye sheria na sera.
3. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Tume ya Kurekebisha Sheria, kufanya mapitio na kuondoa au kurekebisha sheria zote zinazowabagua wanawake na kuwanyima haki zao kinyume na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa iliyoridhiwa na Tanzania.
4. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kufanya mabadiliko ya sheria ili kuondoa ndoa za utotoni kwenye Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, kulingana na hukumu ya Mahakama ya Rufani kwenye kesi ya Rebeca Gyumi ya mwaka 2019, kwa kuweka umri chini wa kuoa na kuolewa kuwa miaka 18.
5. Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, kuongeza bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, ikizingatiwa kwamba matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto yanaongezeka.
6. Wanajamii kujiepusha na tabia ya kuwalinda watuhumiwa wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa sababu tu ya kutaka 'kuficha aibu ya familia.'
7. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Mambo ya Nje, kuridhia Mkataba wa Nyongeza kwenye Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu haki za Watu wenye Ulemavu barani Afrika wa mwaka 2018.
8. Vyombo vya habari kufichua na kuripotia vitendo mbalimbali vya ukiukwaji wa haki za makundi maalum, ikiwemo watu wenye ulemavu.
9. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, kuanzisha mchakato wa kutunga sheria maalum ya kulinda haki za wazee.
10. Serikali, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia, kuboresha mfumo wa elimu ili kuongeza ubora wa elimu

inayotolewa na kuwaandaa vizuri vijana kwa ajili ya ajira na kujiajiri.

11. Serikali, kupitia Wizara ya Afya, kuhakikisha watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanapata huduma bora za afya, ikiwemo upatikanaji wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI.

## Mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu

1. Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Katiba na Sheria, kuimarisha mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa haki za binadamu na kushughulikia changamoto ambazo mifumo hiyo inakabiliana nazo ili kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu.
2. Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Katiba na Sheria, kuhakikisha bajeti ya kutosha inatengwa kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili kukiwezesha chombo hiki muhimu cha ulinzi wa haki za binadamu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.
3. Asasi za kiraia kueneza uelewa wa umma kuhusu mifumo mbalimbali ya kitaifa, kikanda, na kimataifa ya ulinzi wa haki za binadamu.
4. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kusaini upya tamko la kuruhusu asasi za kiria na watu binafsi kufungua kesi katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ili kuongeza upatikanaji wa haki kwa Watanzania.
5. Serikali, kupitia Wizara ya Sheria na Katiba, kuhakikisha kwamba hukumu na mapendekezo yanayotolewa na mifumo ya kikanda ya haki za binadamu, hususan Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Mahakama ya Afika Mashariki ya Haki, inatekelezwa.
6. Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kutekeleza mapendekezo 187 iliyoyakubali katika mchakato wa tathmini ya rekodi ya Tanzania ya haki za binadamu (UPR) iliyofanywa na Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu mwaka 2021.



LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Are you passionate about the protection and promotion of Human Rights?

## Donate Now!

airtel money

**How to Donate (Airtel Money)**

1st Step: Dial *150*60# to access your AIRTEL MONEY account.
2nd Step: Select 5 – Make Payments.
3rd Step: Select 4 – Enter Business Number.
4th Step: Enter business number (275454)
5th Step: Enter the amount you want to pay.
6th Step: Enter the reference number.(1234)
7th Step: Enter your "PIN" to confirm.

tigo pesa

**How to Donate (TigoPesa)**

1st Step: Dial *150*01 # to access your Tigo Pesa account.
2nd Step: Select 4 – Pay Bills.
3rd Step: Select 3 – Enter Business Number.
4th Step: Enter business number (275454)
5th Step: Enter the reference number.(1234)
6th Step: Enter the amount you want to pay.
7th Step: Enter your "PIN" to confirm.

vodacom m-pesa

**How to Donate (M-PESA)**

1st Step: Dial *150*00# to access your MPESA account.
2nd Step: Select 4 – Pay By Mpesa.
3rd Step: Select 4 – Enter Business Number.
4th Step: Enter Business number (275454)
5th Step: Enter the reference number.(1234)
6th Step: Enter the amount you want to pay.
7th Step: Enter your "PIN" to confirm.
8th Step: Enter 1 to confirm the transaction

@humanrightstz You Tube Haki TV

*For a Just and Equitable Society*

**LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE, HEADQUARTERS**
Justice Lugakingira House, Kijitonyama,
P. O. Box 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Tel:** +255 22 2773038/48 **Fax:** +255 22 2773037
**Email:** lhrc@humanrights.or.tz **Website:** www.humanrights.or.tz

---

**THE LEGAL AID CLINIC**
Isere Street – Kinondoni, P. O. Box 79633, Dar es Salaam, Tanzania
**Phone/Fax:** +255 22 27612015/6 **Email:** legalaid@humanrights.or.tz

---

**ARUSHA OFFICE,**
Olerian Street, Plot No. 116/5, Sakina kwa Iddi
P. O. Box 15243, Arusha, Tanzania
**Phone:** +255 27 2544187 **Email:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

---

**DODOMA OFFICE**
Plot No. Area D, P. O. Box 2289, Dodoma, Tanzania
**Phone/Fax:** +255 262350050 **Email:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV